SUPA JACKPOT
TZS.1,033,283,276
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 8

**BUNGE** laingilia ucheleweshaji mafao wastaafu




UKURASA 13

Nipashe
Jumamosi Septemba 24, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581078
www.ippmedia.c...
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashet...
...n.com/theguardian_newspaper
...FOLLOW US

# Kibano kikali bima ya afya



Waziri Ummy Mwalimu




UKURASA 2

UKURASA WA 3

## FAINI BILIONI 5/- KAMPUNI IKIVUJISHA TAARIFA BINAFSI

KIBANO dhidi ya kampuni au shirika linalofanya makosa ya ufichuaji wa taarifa binafsi, ikiwamo kuuza taarifa sasa kinanukia baada ya serikali kupendekeza bungeni kutungwa sheria itakayokuwa na adhabu ya faini isiyopungua...

UKURASA WA 4

## KIONGOZI WA DINI ATAJA MBINU ZA KUKABILIANA NA PANYA ROAD



Kiongozi wa Kanisa la The Word of Reconciliation Ministries, Nabii Nicholous Suguye, ametaja mbinu za kubaini vikundi vya vijana...

UKURASA WA 4

## MKEMIA ADAI HUENDA MWILI ULICHOMWA KABLA KUFUKIWA


MKEMIA Mwandamizi kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Kaijunga Brassy ameiambia mahakama mabaki ya mwili wa marehemu Farihani Maluni, ikiwamo mifupa, hayakuonyesha majibu ya vinasaba kwa sababu ulikuwa...

UKURASA WA 9

## JELA MIAKA 30 KWA KUMNAJISI MWANAWE



MKAZI wa Kijiji cha Kimana, Kata ya Partimbo wilayani Kiteto mkoani Manyara, Charles Lemje (52) amehukumiwa kifungo cha miaka 30 kwenda..



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akihutubia mkutano wa Baraza Kuu la 77 la Umoja wa Mataifa (UNGA), unaoendelea jijini New York, nchini Marekani juzi. **PICHA: OMR**

## CAG amaliza utata wa TRAB na TRAT

UKURASA 2

## Serikali yaweka msimamo bomba la mafuta

UKURASA 3

MICHEZO NABI AWAANDALIA 'SUPRISE' AL HILAL FC UK.32

KABWELA UK. 7



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiongoza waombolezaji kutoa heshima za mwisho kwa mwili wa aliyewahi kuwa Katibu Mkuu Kiongozi, marehemu Balozi Paul Rupia, katika viwanja vya Karimjee, jijini Dar es Salaam jana na baadaye mazishi yake kufanyika kwenye makaburi ya Kinondoni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kibano kikali bima ya afya

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

ADHABU ya kifungo gerezani na faini ya mamilioni itawakumba watu na watoa huduma wa afya nchini wanaodanganya katika matumizi ya vifurushi vya bima ya afya baada ya serikali kupendekeza bungeni kutunga sheria mpya.

Vilevile, inapendekeza kosa lililotendwa na skimu ya bima ya afya au kituo cha kutolea huduma za afya kilichoingia mkataba, kulipa faini isiyopungua Sh. milioni tano na isiyozidi Sh. milioni 100.

Mwanachama au mnufaika wa bima ya afya atakayetenda kosa la kutoa taarifa za uongo na kutiwa hatiani, atapaswa kulipa faini isiyopungua Sh. 200,000 na isiyozidi Sh. milioni moja au kutumikia kifungo kisichopungua miezi 12 au adhabu zote mbili.

Jana Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi, aliusoma kwa mara ya kwanza bungeni jijini Dodoma muswada huo wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2022 kisha Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson, kuelekeza upelekwe kwenye kamati husika kwa ajili ya kuchambuliwa na kujadiliwa na baadaye apelekewe taarifa ya kazi hiyo.

**BILA BIMA HAKUNA HUDUMA**

Muswada huo umeweka zuio la kupata baadhi ya huduma pasipokuwa na huduma ya bima ya afya, ikipendekezwa kuwapo sharti la mtu kuwa na bima hiyo pale anapohitaji huduma kutoka mamlaka zinazohusika na usimamizi au utoaji wa leseni ya udereva, bima za vyombo vya moto na utambulisho wa mlipakodi, usajili wa laini za simu, leseni za biashara, hati ya kusafiria au viza, uandikishaji wa wanafunzi wa kidato cha tano, cha sita na vyuo na utoaji wa kitambulisho cha taifa.

Mamlaka husika zitalazimika kuhakikisha usajili au utoaji wa vibali, hati au leseni kwa waombaji, unazingatia kigezo cha kuwapo uthibitisho wa uanachama katika skimu ya bima ya afya.

Makosa ya jumla kwa mujibu wa sheria hiyo yanapendekezwa kuwa kwa mtu atakayekiuka masharti yeyote ya sheria, akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi Sh. milioni 50 au kutumikia kifungo kisichopungua mwaka mmoja au vyote.

Vilevile, kwenye makosa yatendwayo na taasisi, endapo kosa limetendwa na kampuni au taasisi chini ya sheria hiyo, mkurugenzi, meneja au mbia wa kampuni au taasisi hiyo atawajibika.

Hata hivyo, muswada huo unaelekeza ikiwa atatiwa hatiani kwa sababu iliyoanishwa kuhusiana na kosa hilo, isipokuwa kama mkurugenzi, meneja au mbia huyo ataithibitishia mahakama kwa kiasi cha kuiridhisha kwamba kitendo kilichosababisha kosa hilo kufanyika pasipo yeye kuwa na uelewa, kutoa idhini au kuchukua hatua za makusudi kuzuia kosa hilo kutendeka.

Muswada huo unapendekeza skimu ya bima ya afya kufanya tathmini ya uhai na uendelevu kila baada ya miaka mitatu au wakati wowote kadri itakavyokuwa imeelekezwa na mamlaka kwa kumtumia mtathmini.

Vilevile, muswada huo unapendekeza kila mwajiri chini ya sekta ya umma na sekta rasmi binafsi, kuwasilisha katika skimu, asilimia sita ya mshahara wa mwajiriwa, ambapo ndani yake mwajiri atachangia nusu au zaidi ya kiwango hicho na kiwango kilichosalia kitachangiwa na mwajiriwa.


Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Sky Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O. Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania

Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

**VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA** KUUTANGAZIA UMMA WA WATANZANIA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | AINA NA SEHEMU YA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | CHARLES ODEN MWAIHOLA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – KIBAHA | LEGENDS AUCTION MART | 09-10-2022 |
| 2 | AMON AUGUSTINO MCHOMVU | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – KIMARA | LEGENDS AUCTION MART | 09-10-2022 |
| 3 | PATRICK JULIUS KENDAMVANO | PAGALE | MKATABA WA MAUZIANO – KIBAMBA | JOFORTE AUCTION MART COMPANY | 09-10-2022 |
| 4 | PETER JERE LEMUNGE | GARI | TOYOTA LANDCRUISER PRADO – T 828 DFX | JODAC PROFESSIONALS | 09-10-2022 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika ofisi za wakuu wa wilaya wanaohusika.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

117059902


# CAG amaliza utata TRAB na TRAT

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI imesema haina kesi 1,097 za kodi za muda mrefu zenye thamani ya Sh. trilioni 360 na dola za Marekani milioni 181.4 ambazo hazijaamuliwa huku Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) akifafanua kuhusu suala hilo.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba alitoa kauli hiyo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina ambalo juzi Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson aliagiza lijibiwe upya.

Dk. Nchemba alisema hadi Agosti mwaka huu kulikuwa na mashauri 854 kwenye hatua mbalimbali za usikilizaji yenye kodi inayobishaniwa ya Sh. trilioni 4.21 na dola za Marekani milioni 3.48 katika Bodi ya Rufani za Kodi na Baraza la Rufani za Kodi.

Alikiri taarifa za CAG kuonyesha hilo na kwamba kilichofanyika ni makubaliano kati ya Acacia na serikali, jambo hilo lilipelekwa kwa Kampuni ya Barrick.

"Kipindi cha Hayati MaguAlisema kuwa mengine yalikubaliana mbali na ubia kulikuwa na kesi kati yao na serikali ya dola za Marekani bilioni 2.7 wakafuta na walikubaliana kutoa dola za Marekani milioni 40 kwa ajili ya ujenzi wa barabara.

Alisema walikubaliana watakuwa wanatoa dola za Marekani milioni 10 za ujenzi wa maabara ya madini.

"Kilichofuatia mwaka 2021 tulipokea gawio na mwaka 2022 tulipokea gawio na dola Milioni 300 ambazo ni Sh. bilioni 700, ilikuwa ni sehemu ya makubaliano kwenye mjadala na sherehe ile ilifanyika Ikulu mbele ya Hayati Magufuli," alisema.

**JICHO LA CAG**

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Aprili 12 mwaka huu, CAG Charles Kichere ameligusia suala hilo, akisema hesabu za Mamlaka ya Mapato (TRA) kwa mwaka wa fedha 2020/21 zinaonyesha kuwapo kodi zilizoshikiliwa katika mahakama za rufani kwa muda mrefu Sh. 357,308,998,541,722 (Sh. trilioni 357.309).

Anabainisha kesi 46 za kodi zenye thamani ya Sh. 724,183,356,570 (Sh. bilioni 724.183) zipo katika Mahakama ya Rufani kwa mwaka 2020 na 2021.

"Katika mwaka wa fedha 2018 hadi 2021, kuna idadi ya kesi 176 zenye thamani ya Sh. 1,176,301,825,259 (Sh. trilioni 1.176) katika Mahakama ya Rufaa ya Mapato ya Kodi (TRAT)

"Kesi 847 zenye thamani ya Sh. 355,408,513,359,893 (Sh. trilioni 355.308) zipo katika Bodi ya Rufani ya Mapato ya Kodi (TRAB) za tangu mwaka 2016 hadi 2021. Mwaka 2017 ilikuwa na kiasi kikubwa cha kodi ya Sh. 349,862,963,907,128 (Sh. trilioni 349.863).

"Katika majadiliano niliyofanya ya tarehe 23 Septemba 2021 na TRAB pamoja na TRAT, nilibaini changamoto katika utaratibu wa kusikiliza kesi," anasema CAG na kuzitaja shida hizo zinajumuisha upungufu bajeti uliokwamisha usikilizaji na kufanya uamuzi kwa kesi hizo kwa muda.

CAG anasema kuna rufani za kesi za kikodi 45 zenye thamani ya Sh. 5,594,675,387,242.4 (Sh. trilioni 5.595) na kesi tisa (9) zenye thamani ya Sh. 56,678,445,387.80 (Sh. bilioni 56.678) zilizopo TRAT na TRAB mtawalia.

Anasema ingawa rufani hizo za kesi za kikosi zilikuwa katika mazungumzo (negotiations) kati ya serikali na walipakodi, mazungumzo hayo yamechukua muda mrefu bila kufikia mwafaka.

"Kutokana na majibu ya TRA, hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2021, hali za kesi katika mahakama za rufani za kikodi zipo kesi 866 zenye thamani ya Sh. 5,190,108,141,768 (Sh. trilioni 5.19) zinazohusisha dola za Marekani 248,397,084 zilizobadilishwa kwa Sh. 2,309.24 kwa dola.

"Miongoni mwa kesi za rufani zilizoisha ni kesi 45 zenye thamani ya Sh. 5,594,675,387,242.40 (Sh. trilioni 5.595) ambazo zipo katika mazungumzo kati ya serikali na

kampuni za madini ambayo ni North Mara Gold Mine, Pangea Minerals Limited, Bulyanhulu Gold Mine na ABG Exploration.

"Kuna kesi Na.189 ya mwaka 2017 inayoihusu Bulyanhulu Gold Mine imepinga uamuzi wa kulipa kiwango pungufu cha Sh. 21,395,712,853,964 (Sh. trilioni 21.396) ili kusajili pingamizi la kodi kwa tathmini ya kodi kutokana na kutokuwa na taarifa za walipakodi (Jeopardy Assessment) kwa mwaka 2000-2017 kati ya jumla ya deni la Sh. trilioni 343.5. Kesi hii imetolewa mahakama za rufani za kikodi na kurejeshwa kusikilizwa na TRA," anafafanua.

CAG anaishauri serikali iharakishe mazungumzo (negotiations) na walipakodi kwa kesi zilizo katika mazungumzo," CAG Kichere anawasilisha.

## HABARI KITAIFA

# Serikali yatoa msimamo mradi bomba la mafuta

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetoa msimamo wake kuhusu utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Tanga ikisisitiza hauna athari za kimazingira.Msimamo huo umetolewa baada ya baadhi ya wadau wa maendeleo kuwa na shaka katika utekelezaji wa mradi huo wakihofia kutekelezwa pasi na kuzingatia athari za kimazingira na haki za binadamu.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliyasema hayo bungeni jana alipoahirisha mkutano wa nane wa Bunge la 12 jijini hapa.

Alisema, mradi huo ni muhimu kwa manufaa ya nchi hizo mbili katika kukuza biashara, viwanda vya uzalishaji, kuongeza ajira na kuvutia wawekezaji ambao wanatarajia kukuza teknolojia na ujuzi kwa wananchi.

"Mheshimiwa Rais ana matamanio makubwa ya kuifanya sekta ya nishati kuwa chanzo cha ukuaji wa uchumi na kuboresha sekta nyingine ikiwamo viwanda ambavyo ukuaji wake unategemea zaidi kuwapo nishati ikiwamo mafuta na gesi," alisema.

Alibainisha kuwa, mradi huo umefanyiwa tathmini ya kina ya kimazingira na kuhakikisha utekelezaji wake hauna athari za kimazingira na kwa jamii.

"Mradi huu kwa upande wa Tanzania unagusa watu 9,513 zikiwamo taasisi mbalimbali. Miongoni mwao ni watu 331 pekee ndiyo watakaohamishwa, sawa na asilimia 3.5,"alisema. Waziri Mkuu aliongeza kuwa wanaoguswa na mradi huo walishirikishwa kuchagua kujengewa makazi mapya au kupewa fedha taslimu.

"Asilimia 85 walichagua kujengewa makazi na ujenzi wa makazi hayo unaendelea ambapo nyumba 37 kati ya 309 zimekamilika na kukabidhiwa kwa wahusika. Nyumba 55 ziko kwenye hatua ya umaliziaji na nyumba 217 zipo kwenye hatua za awali za ujenzi," alisema.

Waziri Mkuu alisema, Serikali ya Tanzania inaungana na Serikali ya Uganda kuwahakikishia wadau wote likiwamo Bunge la Umoja wa Ulaya na Jumuiya ya Kimataifa kuwa mradi huo unatekelezwa kwa kuzingatia sheria zote za Tanzania na za kimataifa, uwazi, tahadhari za kimazingira, ulinzi wa mifumo ya kiikolojia na rasilimali za maji, masuala ya kijamii, kijinsia na haki za binadamu kwa ujumla.

"Hivyo, niwatoe hofu wadau wote kuhusiana na utekelezaji wa mradi huu na serikali itaendelea kutumia njia za kidiplomasia kuhakikisha wadau wanapata taarifa sahihi kuhusu utekelezaji wa mradi na uzingatiaji wa viwango vya Kimataifa," alisema.

Akizungumzia mbolea ya ruzuku, Majaliwa alisema hadi kufikia tarehe 31 Agosti, 2022 wakulima 956,920 walikuwa wamesajiliwa kwa ajili ya kupata mbolea ya ruzuku ambapo jumla ya tani 60,882 za mbolea zimenunuliwa na wakulima katika mikoa ya Arusha, Iringa, Mbeya, Morogoro, Njombe, Rukwa, Ruvuma na Songwe.

Waziri Mkuu, pia alisema katika kipindi cha mwaka 2021/2022, tathmini awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula imeonesha uzalishaji wa mazao ya chakula umefikia tani milioni 17.4, ambapo kati yake uzalishaji wa mazao ya nafaka ni tani milioni 9.4 na mazao yasiyo ya nafaka ni tani milioni 7.9.

"Mahitaji yote ya chakula yanayojumuisha nafaka na yasiyo ya nafaka kwa mwaka 2022/2023 ni zaidi ya tani milioni 15 ambapo tani milioni 9.5 ni za mazao ya nafaka na tani milioni 5.5 ni mazao yasiyo ya nafaka. Kwa kulinganisha uzalishaji na mahitaji, nchi yetu ina kiwango cha utoshelevu wa chakula wa asilimia 115," alisema.

Alisema, ili kuhakikisha hali ya chakula nchini inaendelea kuimarika, serikali imeuwezesha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kuhifadhi tani 147,142 na kuendelea kununua mazao ya chakula kwa ajili ya kuhifadhi. Waziri Mkuu alitoa wito kwa jamii, viongozi wa dini na watanzania kuungana kwa pamoja kukemea, kufichua na kudhibiti matukio yote yanayoashiria kuondoa amani na utulivu.

# Faini bilioni 5/- kampuni ikivujisha taarifa binafsi

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

KIBANO dhidi ya kampuni au shirika linalofanya makosa ya uficheuaji wa taarifa binafsi, ikiwamo kuuza taarifa sasa kinanukia baada ya serikali kupendekeza bungeni kutungwa sheria itakayokuwa na adhabu ya faini isiyopungua Sh. milioni moja na isiyozidi Sh. bilioni tano.

Ikiwa ni mtu binafsi atakayebainika kutenda kosa na kutiwa hatiani chini ya kifungu cha 60 (6) (a) cha Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Mwaka 2022, atalipa faini isiyopungua Sh. 100,000 na isiyozidi Sh. milioni 20 au kifungo kisichozidi miaka 10 au vyote kwa pamoja.

Muswada huo wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2022 ulisomwa kwa mara ya kwanza jana bungeni jijini Dodoma na Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi.

Kuhusu makosa ya uharibifu, ufutaji, ufichaji au ubadilishaji wa taarifa binafsi, sheria hiyo inapendekeza atakayetiwa hatiani kwa kutenda makosa hayo, atalazimika kulipa faini isiyopungua Sh. 100,000 na isiyozidi Sh. milioni 10 au kifungo kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Adhabu ya jumla chini ya kifungu cha 63 (b) cha sheria hiyo inaelekezwa kuwa baada ya mtu kutiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya sheria hiyo, mahakama inaweza kuamuru kukamatwa kwa vifaa vyake vyenye taarifa binafsi vilivyohusika katika kutenda kosa.

Pamoja na mambo mengine, sheria hiyo inaeleza kuwa mkusanyaji ambaye bila sababu za msingi, atafichua taarifa binafsi kwa njia yeyote ambayo haiendani na madhumuni ambayo taarifa hiyo imekusanywa, atakuwa anatenda kosa.

Kwamba, atapata taarifa binafsi au atapata taarifa yoyote inayojumuisha taarifa binafsi bila idhini ya mkusanyaji au mchakataji, ambaye anahifadhi taarifa hiyo, atafichua taarifa binafsi kwa mtu mwingine atakuwa ametenda kosa. Na mtu atakayeuza taarifa binafsi, ambayo imepatikana kwa ukiukwaji wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 60 cha sheria hiyo, atakuwa ametenda kosa.

Kwenye sheria hiyo inayopendekezwa, mtu ambaye ataizuia au kuikwamisha Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kutekeleza mamlaka yaliyotolewa chini ya sheria hiyo, kushindwa kutoa msaada au taarifa zilizoombwa na tume, endapo atatiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua Sh. 100,000 na isiyozidi Sh. milioni tano au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**
**BODI YA MFUKO WA BARABARA**

**KUTOA TAARIFA ZA HALI YA BARABARA KWA KUTUMIA MFUMO WA KIELEKTRONIKI**

***Bodi ya Mfuko wa Barabara imeunda Mfumo wa Kielektroniki wa kufuatilia hali ya barabara (e-Monitoring Application). Mfumo huu umeundwa mahsusi kuwawezesha wananchi, hasa watumiaji wa barabara, kushiriki katika kusimamia na kutunza miundombinu ya barabara katika maeneo wanayopita kwa kutuma taarifa muhimu za hali ya barabara.***

**Je ni taarifa gani mtumiaji wa barabara anaweza kutuma?**

Taarifa ambazo mwananchi anaweza kutuma ni pamoja na barabara kujifunga, daraja au kalavati kubomoka au kuzolewa, mashimo hatarishi barabarani, ajali, miti kuanguka barabarani, gari kumwaga oil barabarani, gari kutengenezewa barabarani na wizi au uharibifu wa samani za barabara.


Barabara kukatika


Ajali barabarani


Shimo hatarishi barabarani


Sehemu ya barabara kuzolewa na maji

**Je mtumiaji wa barabara atatuma wapi taarifa hizo?**

Taarifa hizo zitapelekwa kwa Wakala wa Barabara za Kitaifa (TANROADS) na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) pamoja na Bodi ya Mfuko wa Barabara ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. Aidha, mtoa taarifa atapokea mrejesho jinsi taarifa yake itakavyokuwa inafanyiwa kazi.

**Je mtumiaji wa barabara atatumaje taarifa hizo?**

Kupitia Mfumo huo, mtumiaji wa barabara anaweza kutuma taarifa kwa kutumia simu-janja (smart phones) au simu za kawaida (kitochi).

Taarifa hizo zinaweza kutumwa kwa njia ya maandishi, picha au video kutegemeana na aina ya simu.





**Jinsi ya Kupakua App ya Kutolea Taarifa**
1. Fungua "Play Store" au "App Store"
2. Tafuta neno "Barabara"
3. Bonyeza kitufe cha "Install"
4. Subiri mpaka ifike 100%
5. Bonyeza kitufe cha "Open" na uendelee kwa kufuata maelekezo.

**Au tuma taarifa kwa kufuata utaratibu ufuatao:**
1. Piga *152*00#
2. Chagua 4
3. Chagua 5
4. Fuata maelezo.

Je mtumiaji wa barabara atalipia gharama za kutuma taarifa hizo?

Bodi ya Mfuko wa Barabara itagharamia malipo yote ya kutuma taarifa na hivyo mwananchi hatalipa gharama yoyote.

Je maelezo zaidi juu ya Mfumo huo yanapatikanaje?

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na Bodi ya Mfuko wa Barabara kupitia:**

Bodi ya Mfuko wa Barabara,
Makao Makuu Dodoma,
11 Barabara ya AMMAR,
41107 Dodoma Makulu, Dodoma
**Simu :** +255 26 2963277-8
**Nukushi**: +255 26 2963279-80
**Barua pepe:** info@roadsfund.go.tz
**Twitter:** @rfb_tz
**facebook:** www.facebook.com/RFBTZ/
**Instagram:**@rfb_tz

217059602

## TAWA yakiri wanyama wakali tatizo

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), imesema kuongezeka kwa matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu ni moja ya changamoto inayoikabili mamlaka.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Kaimu Kamishna wa Uhifadhi TAWA, Mabula Nyanda, wakati wa mkutano baina ya mamlaka hiyo na wahariri na waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari.

Alisema, kuimarika kwa ulinzi wa rasilimali za wanyamapori kumesababisha kuongezeka kwa mtawanyiko wa wanyama katika maeneo mengi nchini, hivyo kuongeza mwingiliano kati yao na binadamu.

Nyanda alisema, kati ya mwaka 2016/17-2020/21 kulikuwa na matukio 6,472 ya wanyama wakali na waharibifu katika wilaya 85 nchini ambayo yalisababisha watu kupoteza maisha, majeruhi, mifugo kuuawa na mashamba kuharibiwa.

Alisema kwa mwaka 2020/21 pekee jumla ya siku 12,491 za doria zilitumika kukabiliana na matukio 1,706 ya wanyama wakali katika wilaya 85 nchini.

Pia alisema, kumekuwa na wimbi la uvamizi kwa ajili ya shughuli za binadamu ikiwamo, makazi, kilimo, uvuvi na mifugo katika maeneo yaliyohifadhiwa na kusababisha uharibifu wa bionuai.

Aidha, alisema uvamizi huo umesababisha migogoro mingi na uhasama usio wa lazima kati ya mamlaka na wahusika na hata jamii zinazozunguka maeneo yaliyohifadhiwa.

"Mathalani, tatizo hili limekithiri sana katika mapori tengefu likiwamo la Kilombero ambalo ni chanzo kikuu cha maji cha Mto Rufiji ambao maji yake yanatumika katika bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere, Rufiji mkoa wa Pwani," alisema.

Hata hivyo, Nyanda aliishukuru serikali kwa marekebisho ya Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009 ambayo imeweka utaratibu wa kushughulikia masuala ya mifugo inayokamatwa hifadhi kwa muda mfupi. Alitaja changamoto nyingine kuwa ni ongezeko la kampeni za kupinga uwindaji wa kitalii ambazo zimezorotesha ustawi wa tasnia hii na kuutaja mlipuko wa UVIKO - 19 kuwa umeongeza kuzorota kwa uwindaji.

Nyanda alisema, mamlaka itaimarisha uwezo wa taasisi katika kutoa huduma na watumishi watajengewa uwezo kwa kupewa mafunzo stahiki, vitendea kazi, miundombinu wezeshi.

Alisema TAWA, itazingatia maslahi ya kiutumishi ikiwa ni pamoja na maboresho ya mishahara kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Mamlaka.

Vilevile, alisema mamlaka itaweka mifumo madhubuti ya usimamizi wa fedha na kupima matokeo ya utendaji na kwamba pia itafungua kampuni ambayo itafanya biashara ikiwa ni njia ya kuongeza wigo wa mapato.

# Kiongozi wa dini ataja mbinu za kukabiliana na Panya Road

**Na Mwandishi Wetu**

Kiongozi wa Kanisa la The Word of Reconciliation Ministries, Nabii Nicholous Suguye, ametaja mbinu za kubaini vikundi vya vijana vinavyofanya vitendo vya uhalifu, maarufu kama Panya Road.

Moja ya hatua hizo, kwa mujibu wa Suguye, ni jamii kushirikiana na serikali katika kudhibiti vitendo hivyo ili nchi kuwa na amani katika maeneo mbalimbali.

Akizungumza hivi karibuni wakati wa mkutano wa injili uliofanyika jijini Arusha, Nabii Suguye alisema, jamii ina nafasi kubwa ya kuisaidia serikali kukomesha vitendo vya uhalifu kutokana na vijana hao kuwa sehemu ya jamii yenyewe.

"Vitendo hivi vya uhalifu vinafanywa na vijana wadogo ambao bado wanahitaji uangalizi wa karibu wa wazazi au walezi, hivyo kwa kuunganisha nguvu kwa pamoja itasaidia kukomesha vitendo hivi" alisema.

Alisema, jambo la kusikitika ni kuona vikundi vya Panya Road vinaundwa na vijana wadogo ambao ni tegemeo kwa baadaye na kwamba kama jamii itafumbia macho, kutakuwa na wimbi kubwa la vijana wasiokuwa na maadili katika taifa.

"Vijana hawa ni nguvu kazi inayotegemewa katika familia na taifa kwa ujumla. Tusipoamua kuisaidia serikali yetu kwa kukemea na kuwafichua, tutatengeneza kizazi kisichofaa katika taifa na kusababisha hasara kubwa kwenye jamii," alisema.

Kiongozi huyo alisifu kazi kubwa inayofanywa na Jeshi la polisi limekuwa katika kupambana na uhalifu, hivyo wananchi wanapaswa kuliunga mkono kwa kutoa ushirikiano kuwabaini wahalifu hao ili kuendelea kuishi kwa usalama na amani.

Nabii Suguye, alitumia nafasi hiyo kufanya maombezi maalum ya kuiombea nchi na serikali sambamba na kumwombea afya njema Rais Samia Suluhu Hassan, ili aendelee kutimiza majukumu yake. Vikundi vya Panya Road ambavyo vimekuwa vikiibuka na kutoweka mara kwa mara, mapema mwezi huu viliripotiwa kutikisa maeneo kadhaa mkoani Dar es Salaam na kupora vitu mbalimbali kama fedha, simu, kujeruhi na kuua mtu mmoja.

Kutokana na hali hiyo, serikali mkoani Dar es Salaam ilitangaza hatua za kukabili vikundi hivyo vinavyohusisha watoto wa miaka kati ya 11 na 15 ikiwamo kuwakamata na kuwachukulia hatua. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, alitangaza kuwa askari polisi 300 wameletwa mkoani humo pamoja na na magari kadhaa ya doria kwa ajili ya kupambana na uhalifu huo.

Siku moja baada ya kauli hiyo, polisi Kanda Maalum ya Dar es salaam walitangaza kuwaua vijana sita wanaodaiwa kuwa Panya Road, ambao walikuwa katika kutekeleza uhalifu.

Aidha, Bunge pia liliingilia kati na kutaka serikali kuchukua hatua zinazostahili kuhakikisha vitendo hivyo vinakomeshwa haraka. Wabunge pia waliomba kuahirisha kwa muda shughuli za Bunge katika mkutano uliomalizika jana jijini Dodoma ili kujadili suala hilo ambalo pia limeaathiri baadhi yao.




Mtoto mwenye Ualbino, Wande Juma, anayelelewa katika kituo cha Buhangija, Manispaa ya Shinyanga, akitoa shukrani kwa Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (hayupo pichani) juzi, baada ya kuwapatia mafuta maalum kwa ajili ya kinga ya ngozi zao dhidi ya mionzi ya jua na kuwaepusha na ugonjwa wa saratani. **PICHA: MARCO MADUHU**

### KESI YA MAUAJI

# Mkemia adai huenda mwili ulichomwa kabla kufukiwa

**Na Grace Gurisha**

MKEMIA Mwandamizi kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Kaijunga Brassy ameiambia mahakama mabaki ya mwili wa marehemu Farihani Maluni, ikiwamo mifupa, hayakuonyesha majibu ya vinasaba kwa sababu ulikuwa na udhahiri mdogo.

Pia amedai mwili huo ambao ulifukiwa mbele ya nyumba iliyoko Ilala Sharif Shamba inawezekana ulichomwa moto kabla haujazikwa au ardhi aliyozikwa ilikuwa na chumvi, hivyo seli hazikuwa na muunganiko.

Brassy alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Joyce Minde wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakati akitoa ushahidi wake dhidi ya Hemed Ally anayetuhumiwa kumuua Maluni na kumfukia.

Alidai kuwa vielelezo alivyovifanyia uchunguzi huo ni mifupa miwili ya paja, nguo ya ndani ya marehemu, plasta, mifupa ya kwenye kiuno, kamba na nguo yenye vifungo, meno, fuvu la nyuma la kichwa, mkanda, upindo wa suruali na kola ya shati.

Alidai barua ya kufanya uchunguzi wa vitu hivyo pia ilimtaka afanye uchunguzi wa vinasaba vya Abisalum Maluni ambaye ni baba wa marehemu, Faisal na Fahadi (watoto wa marehemu), ambapo aliwachukua mipanyuso mitatu ya kinywa.

Alidai kuwa uchunguzi huo wa vinasaba ulikuwa na lengo la kufananisha mabaki ya marehemu na ndugu hao ili walinganishe vinasaba vyao kama Farihani ni ndugu yao.

Alidai vielelezo hivyo alivipa namba za usajili 115/2015 na baadaye alivihifadhi na akaja kuvifanyia kazi Julai 27/2018 na alibaini kuwa vielelezo namba moja hadi nane havikutoa majibu ya vinasaba.

Hata hivyo, kielelezo namba tisa - baba na watoto wa marehemu vilitoa majibu ya chembe halisi za urithi, katika kulinganisha vilifanana vinasaba vya watoto na baba wa marehemu Farihani.

"Kielelezo namba moja hadi nane yakiwamo mabaki ya mwili wa Maluni havikutoa majibu kwa sababu havikuwa na udhahiri, inawezekana huo mwili ulichomwa moto kabla haujazikwa au ardhi aliyozikwa ilikuwa na chumvi, hivyo seli hazikuwa na muunganiko," alidai.

Awali Brassy alidai Februari 12, 2015 akiwa ofisini, alipokea vielelezo na barua kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Dar es Salaam wakiomba uchunguzi wa vielelezo tisa.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Jumatatu saa tatu asubuhi. Inadaiwa Juni mwaka 2014, Hemed Ally alimuua Farihani Maluni eneo la Sharif Shamba ndani ya Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam.

# Samia ashauri lugha ya Kiswahili kufundishwa Chuo Kikuu Msumbiji

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemshauri Rais wa Msumbiji, Filipe Nyusi, kufanya uamuzi wa kutumia lugha ya Kiswahili katika mfumo wa elimu kuanzia shule za msingi hadi chuo kikuu ili kuimarisha mshikamano kati ya Tanzania na nchi hiyo.

Akuzungumza jana katika kongamano la 12 la Chama cha FRELIMO lililofanyika nchini Msumbiji, Rais Samia alisema kuna sababu mbalimbali za kutumia Kiswahili baada ya nchi hizo kupata uhuru.

Samia, alisema Kiswahili ni lugha sahihi ya kutumia baada ya uhuru wa nchi hiyo na kwamba Tanzania ina kila namna ya kumshukuru na kumpongeza Mwalimu Julius Nyerere kwa kuikuza lugha hiyo.

"Tanzania iko lugha moja ambayo iko juu ya lugha zote. Kiswahili kinaweza kutumiwa kama chombo cha kuwaunganisha Waafrika. Lugha hii ilitumiwa na wapiganaji katika kuwasiliana wakati wa harakati zao za kupigania uhuru. Pia Kiswahili kinaweza kuwaunganisha watu wa Msumbiji," alisema.

"Kutambuliwa Kiswahili kama lugha ya maendeleo ya kusini mwa Afrika, UNESCO (Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni) ilitangaza Julai 7, kila mwaka kuwa Siku ya Kiswahili Duniani. Ningependa kuwaomba watu wote, akiwamo Rais Nyusi, na wajumbe wote waone namna gani ya kufanya uamuzi katika kuiweka lugha ya Kiswahili katika mfumo wa elimu," alishauri.

Samia alisema, Tanzania na Msumbiji zilishapata uhuru kwa sababu waasisi wao walijitoa kwa dhati kwa ajili ya manufaa ya nchi zao, huku akibainisha kwamba bado wana vita vya kupambana na ukoloni ambao uko katika namna mbalimbali.

Pia, alisema kizazi kilichopita kilipambana kupata uhuru wa kisiasa na sasa kinachotakiwa ni uhuru wa kiuchumi. Aliipongeza FRELIMO katika kutafuta maendeleo mbalimbali na kwamba wameshirikiana kupambana dhidi ya ukoloni.

"Wanaposema mapambano yanaendelea ni mapambano halisi na lazima yaendelee. Mapambano yanayotakiwa yajielekeze katika kuimarisha uchumi wa nchi sambamba na vyama ili kufanya kazi vizuri kwa maendeleo makubwa.

"Ili kufanikiwa hilo, tunatakiwa kuwafunza vijana kwenye Chuo cha Mwalimu Nyerere cha CCM Tanzania," alisema.

Pia alisema, amani na utulivu uliopo katika nchi hizo ni kutokana na kuwapo kwa vyama vyao madarakani na kusisitiza kwamba wakati wote panapokuwa na vita hakuna amani.

Alibainisha kuwa, kuna watu wasiowatakia mema ambao wanatoa msaada kuvipa vyama vya upinzani ili wahakikishe vyama vya ukombozi vinakufa na kwamba hakuna chama peke yake ambacho kinaweza kupambana vita hivyo na kusisitiza kufanya kazi kwa ushirkikiano.

# Hatima ya Zumaridi kujulikana Oktoba 4

**Na Pelusy Yohana,** SAUT

UPANDE wa mashtaka katika kesi namba 10 inayomkabili Mchungaji Diana Bundala, maarufu Zumaridi na wenzake wanane, umekamilisha ushahidi wake.

Akihitimisha uwasilishwaji wa ushahidi, vielelezo na kusikiliza mashahidi katika shauri hilo jana, Wakili wa Serikali, Dorcas Akyoo, aliiomba mahakama jana kufunga shauri hilo kwa kuwa hawakuwa na shahidi mwingine.

Mashahidi 12 pamoja na vielelezo, yakiwamo maelekezo ya onyo 11 yalifungwa rasmi jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi mkoani Mwanza.

Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza, Monica Ndyekobora, aliahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 4, 2022 atatoa uamuzi kama washtakiwa wana kesi ya kujibu au la.

"Katika tarehe hiyo mahakama itatoa uamuzi juu ya shauri hilo kama washtakiwa watakuwa na kesi ya kujibu watapata nafasi ya kuwasilisha utetezi wao na endapo hawatakutwa na kesi ya kujibu itajulikana siku hiyo," alisema Ndyekobora.

Mashtaka hayo ya shambulio ni kati ya matatu yanayomkabili mchungaji huyo na wenzake wanane. Mengine ni kudhuru mwili na kuzuia maofisa wa serikali kufanya kazi yao yanayomkabili Zumaridi na wafuasi wake 83 pamoja na ya kutumikisha na kusafrisha binadamu ambayo yanakabiliwa Zumaridi peke yake.

Mshtakiwa huyo pamoja na wenzake walikamatwa mapema mwaka huu eneo la Buhongwa wilayani Nyamagama mkoani Mwanza.


PSSSF
Public Service
Social Security Fund

## TAARIFA KWA UMMA

**Dodoma-Septemba 23, 2022**

Hivi karibuni kumekuwa na taarifa zinazosambaa kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kuhusu viongozi wa PSSSF waliofikishwa kwenye Baraza la Maadili ya Viongozi wa Umma. Taarifa hizo zinazosambaa zimekuwa zikieleza kuwa viongozi hao wamejikopesha mikopo kununua magari binafsi kinyume cha utaratibu.

Tungependa kuufahamisha umma kuwa, taarifa hizo zinazosambaa za viongozi wa Mfuko wa PSSSF kujikopesha fedha kinyume cha utaratibu si za kweli. Bila kuathiri taratibu za uendeshwaji wa mashauri kwenye Baraza la Maadili ya Viongozi wa Umma, Bodi ya Wadhamini imekuwa ikiendelea na utekelezaji wa mikatati ya kupunguza gharama za uendeshaji wa Mfuko ikiwa ni pamoja na kuwakopesha viongozi wa juu wa Mfuko wa PSSSF mikopo ya magari na kuwakata kwenye mishahara yao ya kila mwezi badala ya Mfuko wa PSSSF kuingia gharama za kuwapatia viongozi hao magari ya ofisi, madereva na gharama zingine mbalimbali za matengenezo ya magari hayo. Bodi ya Wadhamini imekuwa ikitekeleza Mkakati huu kwa ufanisi na kwa kuzingatia Sera ya Mikopo na Mamlaka ya Bodi kama yanavyoanishwa kwenye Sheria ya Mfuko wa PSSSF.

Aidha, umma utambue kuwa utaratibu huu si mgeni kwenye Mifuko ya Pensheni nchini kwani ulikuwa ukitumika hapo awali na iliyokuwa Mifuko minne iliyoungana na kuwa Mfuko wa PSSSF. Utaratibu huu ulionesha mafanikio makubwa katika kupunguza gharama za uendeshaji. Hadi sasa, mkakati huu ni miongoni mwa mikakati ya Mfuko inayosaidia kuufanya Mfuko kuwa na gharama za uendeshaji kuwa asilimia 5 ya michango, kiwango ambacho ni chini ya asilimia 10 inayoruhusiwa na Miongozo ya Msimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Tanzania.

PSSSF katika kutimiza matakwa ya utawala bora, ina mifumo madhubuti ya kitaasisi ikiwemo Bodi ya Wadhamini, ambayo ndiyo chombo cha juu cha usimamizi wa Mfuko wa PSSSF chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Hivyo, Bodi katika kutoa mikopo kwa watumishi imekuwa ikizingatia, Sheria ya Mfuko, Sera na Miongozo mbalimbali iliyopo.

Mfuko wa PSSSF unaendelea kutekeleza majukumu yake ya kisheria ikiwa ni pamoja na kulipa mafao. Mfuko umekuwa ukilipa kwa wakati pensheni ya kila mwezi kwa wastaafu kila ifikapo tarehe 25 ya kila mwezi. Aidha, Mfuko kwa sasa unawalipa wastaafu, waliokamilisha taratibu zote, kwa muda uliowekwa kisheria, yaani ndani ya siku 60.

**Imetolewa na**

**James Mlowe**
**Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma**

217059402

Leo.Kesho.Pamoja. www.psssf.go.tz 0800110040 psssftz psssftz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera serikali kusaidia maandalizi Serengeti Girls

**TIMU** ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), inatarajia kuondoka nchini wikendi hii kuelekea Uingereza kuweka kambi maalumu ya wiki mbili kwa ajili ya kujiandaa na fainali za Kombe la Dunia (U-17), zitakazofanyika kuanzia Oktoba 11 hadi 30, mwaka huu huko India.

Hii ni mara ya kwanza kwa Tanzania kupeleka timu kushiriki fainali hizo za dunia na Serengeti Boys imepangwa Kundi D ikiwa pamoja na Canada, Japan na Ufaransa.

Katika kusaka tiketi ya kushiriki fainali hizo, Serengeti Girls inayofundishwa na Kocha Mkuu, Bakari Shime, ilianza kwa kuwaondoa yosso wenzao ndugu zao kutoka Afrika Mashariki na Kati Eritrea, na Burundi na baadaye wawakilishi wa Afrika Magharibi, Cameroon.

Bara la Afrika linawakilishwa na mataifa matatu ambayo ni Nigeria, Morocco na Tanzania inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan.

Serengeti Girls imefika hatua hiyo baada ya kupambana na hii ilitokana na nguvu kubwa iliyoanza kuwekwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), ambalo liko chini ya Rais, Wallace Karia ambaye aliahidi chini ya uongozi wake atahakikisha anatoa kipaumbele kwa soka la vijana na wanawake.

Hatimaye ndoto za Karia na viongozi wenzake zimetimia mwaka huu kwa kufikia malengo ya Watanzania kushiriki mashindano makubwa na kuacha kuwa watazamaji kama ilivyokuwa imezoeleka kwa kipindi kirefu.

Katika kuhakikisha timu hiyo inakwenda India kushindana na si kusindikiza wengine, serikali imegharamia safari ya Serengeti Girls kwenda Uingereza kujifua na hatimaye kuelekea kwenye michuano wakiwa imara.Imeelezwa ikiwa katika mji wa Southampton huko Uingereza, timu hiyo itapata huduma za kiwango cha juu lakini pia itacheza michezo ya kirafiki kwa lengo la kuwajenga wachezaji na kuwaweka tayari kuelekea kwenye mapambano ambayo wametumwa na Watanzania wote.

Lakini mbali na kuisafirisha timu hiyo, serikali imewapatia jezi na vifaa mbalimbali vya mazoezi ili kuzifanya akili za wachezaji hao pamoja na viongozi wa benchi la ufundi wafikiri jambo moja tu la kusaka ushindi na kurejea nyumbani wakiwa mashujaa.

Nipashe linapenda kuipongeza serikali kwa uthubutu ambao imefanya wa kuhakikisha Serengeti Girls wanakwenda katika mashindano wakiwa hawana mawazo ya nje ya uwanja ambayo wakati fulani huchangia kushusha ubora na matokeo ya ndani ya dakika 90.


Tunawakumbusha wachezaji wa Serengeti Girls kuweka mbele uzalendo na kuhakikisha mnakwenda kupeperusha vyema bendera ya taifa na kuiweka Tanzania katika rekodi za juu na zenye heshima.

Ili yote yafanyike kwa ufanisi, wachezaji mnatakiwa kuwa na nidhamu ndani na nje ya uwanja katika kipindi chote cha kuanzia kambini hadi kwenye mashindano, huu ni wakati muhimu sana kwenye maisha yenu lakini pia kwa Tanzania.

Mkumbuke mchezaji atakayefanya vyema kwenye fainali hizo, si tu ataisaidia nchi yake kurejea na taji, lakini pia atajiweka sokoni kwa klabu mbalimbali zitakazokuwa zinafuatilia wachezaji nyota kumsajili na hapo atakuwa amejifungulia milango ya kucheza soka la kulipwa.

Ili mafanikio haya yaliyopatikana yasionekane ni ya kubahatisha, TFF mnatakiwa kuendelea kuwekeza kwa wachezaji hawa vijana ambao baadaye watakapopandishwa kuchezea timu ya wakubwa (Twiga Stars), watakuwa wameiva na wenye uzoefu mkubwa na wataipa mataji Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Sababu ikijulikana, gonjwa la waamuzi nchini litatibika

Na Adam Fungamwango

**MJADALA** uliopo kwa sasa mitaani na katika mitandao mbalimbali ya kijamii ni juu ya baadhi ya waamuzi kuboronga kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hilo limesababisha Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kuwapeleka kwenye Kamati ya Waamuzi, baadhi ya marefa na waamuzi wasaidizi kwa ajili ya kujadiliwa na ikiwezekana kupewa adhabu stahiki.

Waliopelekwa ni mwamuzi bora wa msimu uliopita, Ahmed Aragija na Amina Kyando, huku waamuzi wasaidizi ni Frank Komba, ambaye ni mwamuzi msaidizi bora nchini kwa misimu mitatu pamoja na Black Tubuke.

Mechi zinazohusishwa hapa ni Yanga dhidi ya Azam FC, Prisons dhidi ya Simba na Namungo dhidi ya Coastal Union.

Sitaki kueleza jinsi ilivyokuwa kwani mashabiki wengi wa soka wameona namna waamuzi hawa walivyochezesha, makosa waliyoyafanya na walivyofungiwa.

Labda kwa kuongezea tu naweza kusema Aragija yeye anapelekwa kwa kutomudu michezo yote miwili kati ya Yanga dhidi ya Azam na pia Prisons dhidi ya Simba, wakati Komba yeye alikuwa pamoja na Aragija kwenye mechi ya Yanga dhidi ya Azam. Anadaiwa kutomsaidia vyema mwamuzi wake.

Tubuke yeye alikuwa na Aragija kwenye mechi ya Prisons dhidi ya Simba, naye anadaiwa kumtomsaidia mwamuzi wa kati katika mechi hiyo.

Kwanza niseme hii si mara ya kwanza wala ajabu kwa waamuzi kupelekwa kwenye Kamati ya Waamuzi ili kuadhibiwa kwa makosa ya uwanjani.

Ilitokea na itaendelea kutokea kwa sababu kwenye mpira wa miguu, kama mchezaji anakosea, basi na waamuzi huwa wanakosea.

Hata hivyo, waamuzi wetu wa Kibongo jinsi wanavyokosea wanatia shaka. Kama alivyowahi kusema Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almasi Kasongo mechi hiyo hiyo moja anaweza kumwonya mchezaji wa timu A kwenye kosa, lakini hilo hilo likifanywa na timu B anatoa kadi ya njano.

Ni kwamba makosa yao ya kibinadamu mara nyingi huzinufaisha zaidi timu kubwa, zenye mashabiki na uwezo kuliko ndogo.

Tulisikia hivi karibuni kuna waamuzi watatu tu ambao ndiyo wanaochezesha mechi za timu za Simba na Yanga. Yaani hawa wanazunguka nazo. Nao ni Aragija, Ramadhani Kayoko na Heri Sassi.

Pamoja na taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi, Nassor Hamdoun iliyotolewa ufafanuzi inatokana na sifa zao kwani ni waamuzi kwenye beji ya FIFA na pia ni wazoefu. Ni kweli haipingiki na wala hatukatai, lakini binafsi hili naona ni kosa kubwa.

Kuwepo kwa waamuzi hao hao wanazichezesha timu hizo hizo ni kutengeneza mianya ya rushwa.

Hili suala la rushwa mara nyingi wadau wengi wa michezo huwa wanalikwepa kulitaja hadharani kama halipo, lakini ukizisikia za 'chini ya kapeti' unabaki kupigwa butwaa.

Kwenye nyanja za soka inaonekana watu wanakwepesha sana kuhusu suala hili, lakini hebu angalia katika nyanja nyingine wanavyokuwa makini nalo.

Huwezi kukuta hakimu akikaa kwenye mahakama moja kwa muda mrefu, au askari polisi kuwapo kwenye kituo kimoja kwa miaka mingi.

Hii yote ni kwa sababu ya kukwepa watu hao kuzoeana sana na watu, kitu ambacho kitasababisha utendaji wao kubwa mgumu na hasa wakilenga rushwa. Sasa kama serikali tu inakuwa macho na watendaji wake muhimu hao, sembuse waamuzi kuchezesha timu mbili au tatu tu kila zinakokwenda?

Watoa rushwa watajua tu waamuzi wetu ni hao tu, hivyo ni rahisi 'kucheza nao.'

Inaonekana Shirikisho la Soka Nchini (TFF), na kamati zake za waamuzi wanatoa adhabu kwa waamuzi wanaovurunda, lakini hawatafuti kiini kwa nini wanafanya hivyo. Kama ni hivyo wataendelea kuwafungia.

Binadamu anayeumwa ni lazima kwanza afahamu nini anaugua ndiyo aweze kujitibia.

Inavyoonekana hadi sasa Kamati wa Waamuzi haijajua tatizo ni nini, marefa hawajui kuchezesha, wana mapenzi kwa klabu, wanashindwa kutafsiri sheria kwa makusudi au rushwa, posho hazitoshi au mafunzo wanayotoa ni hafifu?

HABARI KITAIFA

## DC awatangazia vita walimu wakware

**Na Steven William,** IRINGA

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, amewaonya baadhi ya walimu wanaojihusisha na mapenzi na wanafunzi huku akisema huo ni ukatili na watakaobainika watachukuliwa hatua za kisheria.

Amesema vitendo hivyo vinavyofanywa na baadhi ya walimu ni ukosefu wa maadili ya kazi yao na ni ubakaji, jambo ambalo limekuwa likiharibu taswira nzuri ya fani ya ualimu ambayo imekuwa ikiheshimiwa kwa miaka mingi.

Moyo alisema hayo juzi mjini hapa wakati wa kuzindua vitabu vyenye mwongozo wa Waziri Mkuu namna ya kuwapata viongozi katika njia sahihi ambayo haitakuwa na ubabaishaji.

Alisema kumekuwa na baadhi ya walimu wanajihusisha na mapenzi na wanafunzi, hatua ambayo alisema ni ukatili wa makusudi, hivyo akataka walimu kutoa taarifa dhidi ya yeyote atakayekutwa anafanya vitendo hivyo.

Moyo alisisitiza kuwa kazi kubwa ya mwalimu ni kuwafundisha wanafunzi ili kufaulu na kuwa hazina kwa maendeleo ya taifa na si kuwafanyia ukatili.

Kuhusu vitabu hivyo vya mwongozo, alisema vinataka watu wateuliwe kwa kufuata misingi sahihi na si kwa njia za rushwa au kujuana.

Alisema mwongozo huo unapaswa kutumika kulingana na maagizo ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa yanavyotakiwa kuwa na yawe vivyo hivyo.

Naye Meya wa Manispaa ya Iringa, Ibrahim Ngwada, alisema walimu wanafanya kazi kubwa kuwafaulisha wanafunzi licha ya kukabiliwa na changamoto mbalimbali hasa mazingira wanayofanyia kazi. Ngwada alisema halmashauri inatamani kumaliza changamoto zote za walimu hasa kuboresha miundombinu ya kufundishia na mazingira wanayoishi lakini kikwazo kikubwa ni ufinyu wa bajeti.

Alisema wakifanikiwa kupata fedha za kutosha, watakuwa wanatatua changamoto kadiri wanavyoweza ili kuwasaidia walimu kufundisha katika mazingira mazuri.

Awali, akisoma mwongozo huo kwa Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Iringa,

Gerald Mwamuhamila, alisema kitabu cha Mwongozo wa Uteuzi wa Viongozi wa Elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mkoa kinatoa utaratibu wa uteuzi wa viongozi kuanzia ngazi ya shule, kata, halmashauri na mkoa.

Mwamuhamila alisema viongozi wa elimu ni nguzo muhimu katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji, hivyo uteuzi wa viongozi hao hupaswa kufanywa kwa umakini mkubwa kabla ya kuwakabidhi dhamana ya kuongoza.

Alisema mwongozo huo umeunda kamati zitakazoshughulika na uteuzi wa viongozi kuanzia ngazi ya kata hadi ngazi ya mkoa. Alisema kabla ya mwongozo, viongozi wa elimu walipendekezwa na kuteuliwa na kamati ya watu wachache tofauti na itakavyokuwa sasa.



Baadhi ya wadau wa afya wakifuatilia kikao cha kutengeneza mpango kazi wa kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu uchangiaji damu kwa hiari, kilichoitishwa na Wizara ya Afya kupitia Mpango wa Damu Salama, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania yang'ara Afrika ushirikishaji wananchi usimamizi wa wanyamapori

**Na Lusungu Helela**

TANZANIA imetajwa kuwa ni miongoni mwa nchi chache barani Afrika ambazo zinatekeleza dhana ya ushirikishwaji wa jamii katika uhifadhi wa kivitendo kwa kutoa fursa kwa wananchi kushiriki usimamizi rasilimali za wanyamapori

Naibu Katibu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Juma Mkomi, alisema hayo juzi wakati akifungua warsha ya kupitia na kuthibitisha mkakati wa usimamizi na uendeshaji wa maeneo ya Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) iliyofanyika jijini Arusha.

Alisisitiza kuwa WMA ni kinga muhimu kwa maeneo ya Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba, Hifadhi ya Ngorongoro na mapori tengefu.

Mkomi alisema bila WMA, changamoto za kiuhifadhi zitaathiri moja kwa moja hifadhi za taifa, mapori ya akiba, Hifadhi ya Ngorongoro na mapori tengefu


Kutokana na umuhimu huo, Mkomi alitoa wito kwa wadau wa uhifadhi nchini kuendelea kuunga mkono jitihada za serikali za kuendeleza WMA ili kuziwezesha kujisimamia na kujiendesha.

Aliongeza kuwa kupitia ushirikishwaji huo, jamii imekuwa ikinufaika na matunda yatokanayo na shughuli za uhifadhi katika maeneo yao kwa kujiletea maendeleo na huduma za kijamii zikiwamo shule na zahanati. Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori, Dk. Maurus Msuha, amesema toka kuanzishwa kwa dhana ya WMA, jamii imekuwa ikishiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori hali inayopelekea ulinzi kuwa madhubuti.

Alisema kutokana na hali hiyo, maeneo ya WMA yamekuwa yakivutia shughuli mbalimbali za uwekezaji kwa ajili ya utalii wa picha, uwindaji wa kitalii na uwekezaji kwa ajili ya hewa ya ukaa.

Akizungumzia manufaa ya ushirikishwaji huo, Dk. Msuha alisema katika kipindi cha mwaka 2016 hadi 2021 jumuiya 15 zenye mikataba ya uwekezaji katika uwindaji wa kitalii zimekusanya Sh. bilioni 4.91 ambazo zimewezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo ufadhili wa wanafunzi kusoma katika vyuo vikuu.

## KABWELA



## Bil 3/- kufufua reli Manyoni-Singida

SERIKALI kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC), katika bajeti ya mwaka 2022/23 imetenga Sh. bilioni 3.45 kwa ajili ya kufanya tathmini na maadalizi ya awali ya kufufua njia ya Manyoni-Singida yenye urefu wa kilomita 115 ambayo ilifungwa takriban miaka 30 iliyopita.

Lengo la kufufua njia hiyo ni kuboresha usafirishaji wa mizigo na abiria pamoja na kukuza uchumi wa maeneo hayo.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, alibainisha hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu.

Mbunge huyo alitaka kujua lini serikali itarudisha huduma ya treni Manyoni-Singida.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema kwa sasa serikali kupitia TRC, inaendelea na mchakato wa kuwapata makandarasi watakaofanya tathmini ya mahitaji na maandalizi ya awali ya kutekeleza mradi huo.

Mbunge Mtaturu, pia aliishukuru serikali kwa kutoa majibu yenye matumaini kwa wananchi wa Singida, lakini akahoji mpango wa serikali kujenga kwa kiwango cha reli ya kisasa (SGR) ili iwe na uwezo wa kubeba mizigo.

Akijibu swali hilo, naibu waziri huyo alisema kiasi hicho cha fedha ni kwa ajili ya ukarabati wa tuta pamoja na makaravati na uwekaji wa tabaka la kokoto na maboresho mengine.

"Tutajenga kama ambavyo waliboresha reli ya kutoka Tanga hadi Arusha kupitia Moshi kwa maana ya kutumia force account (mfumo wa kutumia nguvu kazi ya ndani), kwa jitihada zako na wabunge wengine, serikali mara baada ya kufanya ukarabati huu wa awali ndipo itafanya tathmini na upembuzi yakinifu kwa ajili ya SGR," alisema.

# Bunge laingilia kadhia ucheleweshaji mafao

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amesema ofisi za wabunge zinapokea malalamiko mengi ya wastaafu nchini kutokana na kusotea mafao yao.

Kutokana na angalizo hilo, serikali imesema ndani ya miezi mitatu itaeleza bungeni namna ya kumaliza tatizo la waajiri kutopeleka michango ya wafanyakazi wao kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii, jambo ambalo limekuwa kero kwa wastaafu kutopata mafao yao kwa wakati.

Akizungumza bungeni jana, Spika Tulia alitoa ushuhuda wa kuwapo wastaafu wanaofuatilia mafao kwa zaidi ya miaka miwili wanaambiwa michango yao haijafika katika mfuko.

"Kama ni kazi ya mwajiri kupeleka mfuko unajua hajapeleka, si kazi yao wastaafu, mfuko unapaswa kumlipa mafao wao wakatafute fedha zilipo, mimi mwajiriwa hii siyo kazi yangu, kwani hata kumwadhibu asipopeleka siwezi, ni kazi ya mifuko kufuatilia fedha hizi," alisema.

Alikumbusha kuwa, sheria inaelekeza mwajiri asipowasilisha michango kuna riba na kwamba wananchi hawapaswi kuteseka kwenye hilo.

"Ninyi serikali mtengeneze utaratibu mzuri wa kuisimamia mifuko itafute fedha na iwalipe wastaafu na wastaafu wasiwe wanateseka," aliagiza.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu ambaye ana dhamana ya kusimamia mifuko hiyo, Prof. Joyce Ndalichako, alikiri kuwapo tatizo la waajiri kutopeleka michango ya wafanyakazi kwenye mifuko na kusababisha wastaafu kutopata mafao kwa wakati au kupunjwa mafao.

"Nilihakikishie Bunge serikali imeliona hili na inalifanyia kazi ili kupata ufumbuzi kwa waajiri ambao madeni yao yamekuwa ya muda mrefu. Kuna wengine imefika miaka 10, kwa hiyo nihakikishe Bunge serikali inafanyia kazi na ndani ya miezi miwili au mitatu tutaeleza namna ya kumaliza tatizo hili ambalo limekuwa la muda mrefu," alisema.

Awali Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Anastazia Wambura, alihoji lini wastaafu ambao waajiri wao walikuwa hawatoi michango katika mifuko ya hifadhi ya jamii watalipwa haki zao.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Patrobas Katambi, alisema mafao ya pensheni hulipwa kwa mstaafu kwa kuzingatia kipindi kilicholipiwa michango yake.

"Kumekuwapo kero baadhi ya waajiri kushindwa kuwasilisha michango ya watumishi wao katika mifuko ya hifadhi ya jamii kwa wakati.

Kutokana na shida hiyo, mifuko imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ikiwamo kuwapeleka mahakamani," alisema.

Alibainisha kuwa mifuko imeingia makubaliano maalum na waajiri 63 namna ya kulipa madeni yao huku 123 wakifikishwa mahakamani baada ya kukaidi kuwasilisha michango kwa wakati.



Waziri Mkuu Kasimu Majaliwa (kushoto), akimsikiliza Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, baada ya kuahirisha Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbunge abaini shida mfumo wa haki jinai




**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Neema Lugangira, ameitaka serikali kupitia upya mfumo wa haki jinai ili kupunguza tatizo la idadi kubwa ya mahabusu kuliko wafungwa magerezani.

Akiuliza maswali bungeni jana, Lugangira alisema mwaka jana Bunge lilitunga sheria ya kuzuia ukamataji kabla ya kukamilisha upelelezi, jambo ambalo halijatekelezwa.

"Je, serikali haioni umuhimu wa kurekebisha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ili kuweka ukomo wa upelelezi kama ilivyo Zanzibar na nchi jirani?" alihoji.

Mbunge huyo pia alihoji kama serikali haioni umuhimu wa kuweka masharti nafuu ya dhamana kwa watu ambao hawana mali kwa kuwa hivi sasa masharti ni makubwa kuliko makosa kama vile kuwakomoa wananchi.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete kwa niaba ya Wizara ya Katiba na Sheria, alisema serikali imeendelea kuhakikisha maboresho ya mfumo wa haki jinai nchini yanafanyika ili kuimarisha upatikanaji wa haki jinai ikiwamo kuondokana na mlundikano wa mahabusu katika magereza.

Kutokana na umuhimu huo, alisema wizara imeandaa andiko la mapendekezo ya maboresho ya mfumo wa haki jinai kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa haki jinai nchini.

"Andiko hilo limewasilishwa kwa wadau wa haki jinai ili kupata maoni ya namna ya kuboresha mfumo wa haki jinai nchini.

"Wadau hao ni pamoja na taasisi za serikali, asasi za kirai, taasisi zisizo za kiserikali, taasisi za dini na vyuo vinavyotoa elimu ya sheria," alisema.

Aliongeza kuwa, wizara imepokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali na yamejumuishwa kwenye andiko hilo.

Akitoa majibu ya nyongeza, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, alisema katiba ya nchi na sheria zipo wazi kuhusu masuala ya haki jinai.

"Hivi karibuni tulikuwa na tatizo la 'panya road' (vijana wahalifu wa mitaani) sasa inavyosema kama vile polisi wasikamate hadi upelelezi upatikane, tulishaweka wazi kwa baadhi ya makosa ya kawaida kama upelelezi haujakamilika hakuna haraka ya kukamata mtu, lakini hili suala la haki jinai lina pande mbili," alisema.



## Jela miaka 30 kwa kumnajisi mwanawe

**Na Jaliwason Jasson,** KITETO

MKAZI wa Kijiji cha Kimana, Kata ya Partimbo wilayani Kiteto mkoani Manyara, Charles Lemje (52) amehukumiwa kifungo cha miaka 30 kwenda jela kwa kosa la kumnajisi mtoto wake mwenye umri wa miaka saba (jina limefadhiwa).

Hukumu hiyo ilitolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Kiteto, Mosi Sasy baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili na mahakama hiyo kujiridhisha kwa ushahidi pasi na kuacha shaka.

Hakimu huyo alisema mshtakiwa alitenda kosa hilo Septemba 23 mwaka jana na mahakama hiyo imemtia hatiani baada ya kusikiliza mashahidi watano wa upande wa mashtaka na utetezi ambapo mshtakiwa huyo alijitetea mwenyewe.

Hakimu huyo alisema mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo katika Kitongoji cha Pori namba moja katika Kijiji cha Kimana Septemba 23 mwaka jana.

Akizungumza mahakamani huko, hakimu alisema mshtakiwa alitenda kosa hilo kinyume cha kifungu cha 130(1)(2)(e) na kifungu cha 131 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura 16.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Wilfred Mollel, aliiomba mahakama kutoa adhabu kali ili iwe fundisho kwa watu wengine katika jamii kufanya kitendo kama hicho.

Mshtakiwa Lemje aliiomba mahakama kumpunguzia adhabu kwa kuwa ni mzee na anaamini hatoweza kuishi maisha ya gerezani.

Baada ya kusikiliza utetezi wa mshtakiwa na ombi la upande wa mashtaka, hakimu huyo alimtia hatiani mshtakiwa huyo na kutoa adhabu ya kifungo cha mika 30 gerezani, akisema vitendo vya ubakaji na unajisi vimekithiri wilayani Kiteto.

# Hakuna kesi kupinga ushindi wa Ruto Mahakama ya Afrika

**Na Allan Isack,** ARUSHA

RAIS wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (AfCHPR), Jaji Iman Aboud, amesema mahakama hiyo haijapokea ombi la upande ulioshindwa uchaguzi au wananchi kuiomba kupitia mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa Kenya na kutoa uamuzi.

Hivi karibuni Mahakama ya Juu ya Upeo ya Kenya ilibariki ushindi wa William Ruto kuwa Rais wa nchi hiyo kwa kipindi cha miaka mitano, lakini kwenye mitandao ya kijamii kukawa na taarifa iliyodai Raila Odinga na wafuasi wake watakwenda (AfCHPR) kwa kuwa hawakuridhika na matokeo ya uchaguzi huo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari mahakamani huko wakati wa utoaji wa uamuzi wa hukumu 18 za mashauri mbalimbali, Jaji Iman alisema hawajapokea ombi kutoka kwa wananchi au walioshindwa uchaguzi huo kwa kuwa nchi hiyo siyo mwanachama wa mahakama hiyo.

"Kwa sababu uamuzi ule ulitolewa na Mahakama ya Juu ya nchi hiyo, lakini ingekuwa nchi ya Kenya wameleta tamko lao, kwamba wako tayari kuwaruhusu wananchi na taasisi zisizokuwa za kiserikali kuleta mashauri yao hapa, wangeleta shauri hilo.

"Lakini kwa sababu Kenya hawajakuwa miongongi mwa nchi za Afrika ambazo wameleta au kuweka matamko yao kutaka kuwaruhusu wananchi na taasisi mbalimbali kuleta mashauri yao hapa na hawawezi kufanya hivyo, labda kama watapitia katika Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kwa kuwa wakipeleka huko watasikilizwa, pia wakiona kuna haja ya kuleta huku italetwa," alifafanua.

Katika hatua nyingine, jaji huyo alisema mahakama hiyo ilihitimisha kikao chake cha 66 walichokaa kwa muda wa wiki nne na kutoa hukumu 18 zikiwamo hukumu ndogo na zile ambazo zinakwenda katika kiini cha shauri husika.

"Tumefanikiwa kutoa hukumu 17 na amri moja, kwa kweli tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa katika kikao hiki tumetoa hukumu nyingi sana na imeweka rekodi kwa kuwa tumefanya kazi kama timu na tumezingatia misingi yetu kama majaji.

"Hukumu nyingi zilikuwa zinahusu masuala mbalimbali yakiwamo ya watu waliofukuzwa kazini na walipeleka kesi katika mahakama za nchi zao na hawakuridhika, hivyo wakaona walete hapa na kesi nyingine zilizokuwa za uchaguzi," alisema.

Hata hivyo, rais huyo alisema utekelezaji wa hukumu za mahakama hiyo siyo wakuridhisha kwa kuwa nchi wananchama wa Umoja wa Afrika ambao hukumu zinatolewa dhidi yao utekelezaji wao umekuwa wa kusuasuala.

"Kwa kuwa tunaamini mahakama hii imeanzishwa na nchi hizo kwa nia nzuri, wanaweza kuweka mikakati ya kutekeleza hukumu za mahakama hii," alisema.



Majaji wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, wakitolea maamuzi kesi 17, jijini Arusha jana, hatua ambayo haijawahi kufikiwa tangu kuanzishwa kwa mahakama hiyo. Wa (pili kushoto) ni Rais wa Mahakama hiyo, Jaji Imani Aboud. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

# Trafiki yataja kiini cha ajali magari ya serikali

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

MKUU wa Usalama Barabarani wilayani Longido mkoani Arusha, Jashi Paul amesema ajali nyingi zinazotokana na magari ya serikali zinasababishwa na mwendo kasi na madereva kutozingatia sheria za usalama barabarani.

Amesema baadhi ya madereva wa serikali wamekuwa hawatii sheria kwa kuamini kuwa wao ni watumishi wa umma, hivyo kuamini wana kinga kuchukuliwa hatua na hivyo kuendesha magari kinyume cha sheria.

Katika ufafanuzi wake kwa Nipashe jana mjini hapa kuhusu suala hilo, Paul alisema madereva hao wanapokiuka sheria za usalama barabrani wanaandikiwa faini ambazo wanatakiwa kuzilipa hapo hapo, akisisitiza kuwa ni aibu kwa gari la serikali kuandikiwa faini.

Alisema marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani ya mwaka huu yametoa mamlaka kwa magari ya dharura kuwa barabarani kwa kazi maalum.

Alitaja magari hayo ni pamoja na ya kubeba wagonjwa mahututi, magari ya kijeshi, misafara ya viongozi wakubwa ukiwamo msafara wa Rais, hivyo aliwataka madereva kupisha magari hayo pindi wanapokutana nayo.


"Ajali nyingi wilayani hapa ni za wanyamapori kugongwa wakiwamo twiga, pundamilia na swala na ajali ni chache kwa kuwa tunakuwapo mpakani na usalama wa barabarani ni mzuri kwa kuwa hatuna matukio ya ajali za mara kwa mara,"alisema Jashi.

Mkaguzi wa Magari wilayani humo, Godluck Banele, aliwataka madereva hao kufanya ukaguzi wa magari kabla ya kuanza safari ili kuepuka ajali zisizokuwa na ulazima.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Longido, Khamana Simba, alikemea vitendo unywaji wa pombe kwa madereva wakati wakitekeleza majukumu yao na akawataka kuwa na siri kwa taarifa za viongozi na watumishi mbalimbali wanaowaendesha.

"Ukiona kiongozi unayemwendesha amepigiwa simu, mko naye kwenye gari, akakwambia usimamishe gari ili ashuke kwenda kuzungumza na simu hiyo, unapaswa kutambua kuwa hutoshi kabisa na unatakiwa kujitafakari," alionya.

Mwakilishi wa Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wilayani humo, Mpela Mwinamila, aliwataka madereva kuacha tabia ya kuchagua kazi wanapopangiwa majukumu na viongozi wao kwa kuangalia kazi zenye posho zisizokuwa na posho wakizikataa kwa sababu zisizokuwa na maana.





## Shirika lavalia njuga utunzaji wa mazingira

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Utunzaji wa Mazingira la Hakimama, limesema jukumu la utunzaji wa mazingira ni la kila mwananchi na kuwataka kujijengea tabia ya kupanda miti kila wakati ili kukabiliana na mabaliliko ya tabia nchi.

Pia limewataka wananchi kuwafundisha watoto kupanda miti katika maeneo yanayozunguka nyumba ili kuwajengea utamaduni wa kuyapenda mazingira na kuyatunza kwa maendeleo endelevu.

Msemaji wa Shirika hilo, Nderingio Mringo, alisema hayo katika mkutano wa wenyeviti wa vijiji 17 vinavyozunguka Mlima Kilimanjaro upande wa Halmashauri ya Moshi. Alisema jukumu la kutunza mazingira si la serikali pekee bali kila mwananchi ana wajibu wa kutunza.

Mringo alisema mabadiliko ya hali ya hewa yanayotokea hivi sasa ni kutokana na uharibifu wa mazingira na kuwataka wenyeviti kutoa elimu kwa kila mwananchi kutunza mazingira.

"Ili kupambana na mabadiliko ya hali ya hewa yaliyoko kwa sasa ni jukumu la kila mwananchi kuhakikisha anatunza mazingira kwa kupenda mazingira katika maeneo tunamoishi," alisema Mringo.

Msemaji huyo pia alisema lengo la kuanzishwa kwa shirika hilo ni kutunza mazingira hususani kurudisha uoto wa asili kuzunguka Mlima Kilimanjaro.

Alisema shirika hilo limeendelea na mpango wake wa kupanda miti ya asili katika maeneo mbalimbali ikiwamo vyanzo vya maji ambapo kwa mwaka huu wamejiwekea lengo la kupanda miti 10,000.

Pia aliwataka wenyeviti wa vijiji kuhakikisha wananchi hawafanyi shughuli zozote za kibinadamu ikiwamo kilimo katika maeneo ya vyanzo vya maji ili kuepuka vyanzo hivo kukauka.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mamba Kaskazini, Nelson Minja , alisema bado kuna umuhimu wa serikali kuendelea kuelimisha jamii juu ya utunzaji wa mazingira kwa lengo la kukabiliana na tabia nchi.

"Kila kikao kinachofanyika kuanzia serikali ya kitongoji hadi taifa kuna haja ya umuhimu wa kuendelea kuhamasisha juu ya upandaji na utunzaji wa miti. Pia Baraza la madiwani litunge sheria ndogo ndogo zitakasosaidia kila kaya kupanda miti 10 na kuitunza pamoja na kuwa na ukaguzi wa kila miezi mitatu," alisema.

# CCM yaonya wagombea michezo michafu

**Na Anjela Mhando,**SIHA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, kimewaonya wanachama na makada wake, waliomba nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya chama hicho kutokana na kukiuka maadili na kanuni.

Pia chama hicho kimewatahadharisha waliogombea nafasi hizo kujiepusha na vitendo vya rushwa na kwamba atakayebainika atachukuliwa hatua za kinidhamu dhidi yake.

Onyo hilo, lilitolewa jana na Katibu wa CCM wa Wilaya ya Siha, Ally Kidunda, wakati akizungumza na vyombo vya habari kuhusiana na uchaguzi unaoendelea ndani ya chama katika ngazi mbalimbali zikiwamo jumuiya.

Katibu huyo aliwataka wanachama na makada hao kuacha kufanya kampeni za kuchafuana kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi na kusisitiza kuwa hawatasita kuwachukulia hatua wale watakaobainika kwenda kinyume cha kanuni za chama.

Vilevile aliwataka Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Uchaguzi wa Jumuiya ya Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM), kuchagua viongozi watakaoleta tija kwenye chama na kuacha kufuata mkumbo.

"Ni kweli ratiba ya uchaguzi imeanza Septemba 23 kwa Jumuiya ya Vijana, Septemba 24 itakuwa ya Umoja wa Wanawake (UWT) na Septemba 25 itakuwa Jumuiya ya Wazazi.

"Uchaguzi wa chama wilaya unatarajiwa kufanyika Oktoba Mosi, hivyo ni lazima kufanya kampeni za kistaarabu bila kumchafua mtu na kuchagua viongozi wenye upeo wa maendeleo na kusaidia wananchi," alisema Kitunda.

Pia alitumia fursa hiyo kukemea vitendo vya rushwa kwa kuwa ni jambo baya litakalosababisha kupata viongozi ambao si wazuri na endapo watabainika hata kama mtu ameteuliwa kuwa mgombea anatumia rushwa, hatua kali zitachukuliwa.

"Kikubwa naomba tuchague viongozi wazuri watakaosimamia ilani kwa kuisimamia serikali kutatua matatizo ya wananchi yanayowakabili na kuleta maendeleo," alisema.

Baadhi ya wanachama wa CCM wilayani humo, akiwamo Wema Bura, wametaka wajumbe hao kuchagua viongozi wazuri ambao wakiona matatizo ya wananchi wanayafanyia kazi mara moja kama ilani inavyowataka na si kuona matatizo na kuyafumbia macho.



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Halima Bulembo (wa tatu kushoto), akikabidhi kitabu cha mwongozo wa uboreshaji elimu ya msingi na sekondari kwa Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Edward Mgaya, baada ya kukizindua wilayani humo jana. Wengine ni Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu, Moses Kisiki (wa pili kushoto), Ofisa Elimu ya sekondari wa wilaya, Fredence Serapion (wa tatu kulia) na Ofisa Elimu ya shule za msingi wa wilaya, Pilly Maxmilian. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Tatizo umbali mrefu wanafunzi basi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANAFUNZI wanaoishi katika Kata ya Kindi, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, wanatarajia kulipa kisogo tatizo la kutembea umbali mrefu wa kilomita 17 kwenda shuleni na kurudi nyumbani baada ya kujengewa shule ya sekondari katika kata hiyo.

Shule hiyo imejengwa katika Kijiji cha Katanini na hadi sasa tayari madarasa manne yamekamilika na matundu 16 ya vyoo na zaidi ya Sh. milioni 264 zimeshatumika kutekeleza ujenzi huo. Fedha hizo zimetolewa na shirika lisilo la kiserekali la FT Kilimanjaro, lililo chini ya Kiwanda cha Sukari (TPC).

Akizungumza na Nipashe, Meneja wa Shirika hilo, Kuya Nangai, alisema wameamua kuanzisha mchakato huo kwa lengo kuondoa adha kwa wanafunzi waliokuwa wakitembea umbali mrefu kwa kuwa baadhi yao ni wanafunzi wa kike ambao wamekuwa wakishindwa kufikia ndoto zao kwa kupata ujauzito kutokana na vishawishi wanavyokutana navyo njiani wakitoka shuleni na wakienda.

Nangai alisema kutokana na umbali huo, wazazi na walezi walikuwa wanashindawa kufuatilia mienendo ya watoto wao. Hatua hiyo pia ilisababisha kiwango cha ufaulu kutoridhisha kwa kuwa wanafunzi walikuwa wanakosa muda wa kusoma.

"Sisi tumejenga vyumba vinne, vyoo na jiko. Tunashukuru serikali na wananchi wameendelea kutuunga mkono kwa kujenga vyumba vingine vinne pamoja na maabara ambayo inaendelea kwa sasa. Hii itasaidia kupatikana kwa elimu bora na kuwapa wazazi na walezi fursa ya kufuatilia matokeo ya watoto wao," alisema.

Akizungumza kwa njia ya simu, Mbunge wa Moshi Vijijini, Prof. Patrick Ndakidemi, alisema kukamilika kwa shule hiyo kutaleta ahueni kwa wanafunzi kutokutembea umbali mrefu kwa kuwa walikuwa wakipoteza muda mwingi kutembea barabarani.

"Tunashukuru kwa mchango huu wa TPC na FT Kilimanjaro wamewasaidia watoto wetu. Walikuwa wakitembea umbali mrefu kwenda na kurudi shuleni na niwaahidi kuwa na sisi tutaongeza nguvu pale mtakapoishia," alisema.

Alisema kata za Kindi na Weruweru, zilikuwa zimesahaulika katika mchakato wa kuanzishwa shule za sekondari kwa kila kata, hivyo kusababisha wanafunzi waliofaulu kutoka ukanda huo kwenda sekondari ya TPC ambayo iko umbali mrefu na pia kulikuwa na adha ya usafiri hasa kipindi cha masika.

Mmoja wa wakazi wa Kindi, Gerson Mshio, alisema kukamilika kwa shule hiyo mbali na kwenda kuwanusuru watoto wa kike na kupata ujauzito pia ufaulu utaongezeka





## Samia atunukiwa tuzo na wahandisi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, ametunukiwa nishani na Wahandisi na Mafundi Sanifu Vifaa Tiba Tanzania (AMETT), kutokana na serikali anayoiongoza kutoa fedha nyingi katika teknolojia ya vifaa tiba.

Nishani hiyo ilipokewa juzi kwa niaba yake na Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, kwenye mkutano mkuu wa AMETT uliofanyika jijini hapa.

Dk. Mollel, alisema nishani hiyo ni heshima kubwa kwa Rais kwa kuwa amefanya kazi kubwa kwenye sekta ya afya kwa kuwekeza kwenye vifaa tiba.

Alisema, kutokana na kuwekeza kwenye eneo hilo zaidi ya watoto 500 wametibiwa hapa nchini na kuokoa zaidi ya Sh. bilioni 17 ambazo zingetumika kuwapeleka kupata matibabu nje ya nchi.

Aidha, alisema huduma za CT-Scan kwa sasa ipo Hospitali zote za Rufani na Kikanda.

"Tiba dawa ya mionzi ilikuwa inaenda kuchukuliwa Afrika Kusini lakini leo tuna kiwanda cha kutengeneza mionzi tiba ambayo ipo pale Ocean Road. "Hayo wenzetu wameyatizama wakasema ni lazima Rais wetu wamshukuru na kumpongeza kwa kazi kubwa.

"Sasa sisi ambacho tunawaomba kwa huu mwaka mmoja amewekeza zaidi ya Sh.bilioni 200 kwenye mikono yao wanakazi kubwa ya kusimamia vifaa hivyo," alisema.

Naibu Waziri huyo aliagiza waganga wakuu wa mikoa na wakurugenzi wa hospitali za Taifa, Kanda, Mikoa na Wilaya kuhakikisha wanapofanya ununuzi wa vifaa tiba wataalamu hao washirikishwe.

"Tukikuta vifaa vimenunuliwa na wataalamu hawajashirikishwa hilo ni tatizo msikae nyuma simamieni eneo lenu," amesema.

Naye Mkurugenzi wa Huduma za Uchunguzi na HTCTS, Alex Magesa, aliomba kuundwa Bodi ya taaluma ya vifaa tiba na kuongeza idadi ya waajiriwa.

# Bunge lataka kasi mradi wa maji Nzuguni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji imeitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), kukamilisha haraka mradi wa maji Nzuguni ili kupunguza makali ya mgawo wa huduma hiyo uliopo sasa.

Pamoja na hayo, imepongeza jitihada mbalimbali za Wizara ya Maji na mamlaka hiyo za kuimarisha upatikanaji wa maji jijini hapa kutokana na ongezeko la watu baada ya serikali kuhamia Dodoma.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dk. Christine Ishengoma, aliyasema hayo jana baada ya wajumbe wa kamati hiyo kutembelea mradi huo.

"Mpaka sasa makao makuu hapa Dodoma walikuwa na shida sana ya maji. Tunaona serikali inajitahidi kutatua tatizo hili na kabla ya miezi sita mradi utakamilika ili kupunguza adha kwa wananchi," alisema.

Dk. Ishengoma, alisema mradi huo utaongeza wingi wa maji kwa Dodoma kutokana na ongezeko hilo.

Naye Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema kutokana na kuwapo kwa uhitaji mkubwa wa maji hasa maeneo ya pembezoni mwa Jiji na Wizara ilielekeza watendaji wa mamlaka watafute popote maji yalipo.

"Nishukuru kazi kubwa imefanyika inatupa matumaini eneo hili la Nzuguni, Ilazo na Kisasa maeneo ambayo yameathirika kwa kiasi kikubwa na upatikanaji wa maji lakini uhitaji wake ni lita milioni nne. Kwa eneo hili la Nzuguni, tumechimba visima vitano vyenye ujazo wa lita milioni sita, hivyo ni toshelevu kwa ajili ya wananchi hawa," alisema.

Waziri alisema, serikali itahakikisha fedha zinatoka kwa wakati na wizara haitakuwa kikwazo kwenye utekelezaji wa mradi huo.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA, Mhandisi Aron Joseph, alisema mradi huo utagharimu Sh. bilioni 4.05 na utanufaisha wananchi 33,969.

Joseph alisema, mradi utaongeza uzalishaji wa maji safi kutoka wastani wa lita milioni 67.8 hadi milioni 73.8 kwa siku sawa na ongezeko la asilimia tisa.

Mkurugenzi huyo alisema, ongezeko hilo litapunguza kwa asilimia tano mahitaji ya maji ya sasa ambayo ni lita milioni 133.8 kwa siku.

"Mgawo wa maji utaondoka kwenye maeneo ya Nzuguni, Ilazo na Kisasa, pia tutapeleka maeneo mengine ya Njedengwa , Mwangaza, Mapinduzi, Iyumbu, Mlimwa, Swaswa na Ipagala," alisema.

Hata hivyo, alisema ili kulinda chanzo cha maji kwenye eneo hilo, Halmashauri ya Jiji la Dodoma inatarajiwa kufanya uthamini wa eneo hilo ambalo bado linamilikiwa na wananchi ili kuwalipa fidia.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (kulia), akimkabidhi Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), Prof. Sebastian Chenyambuga, baadhi ya nyaraka za taasisi hiyo, baada ya kuizindua rasmi, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Waziri aitwisha zigo bodi utafiti mifugo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ameitaka Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) kushiriki kikamilifu katika utafiti utakaoleta tija kwa wafugaji wakati serikali ikielekea kuwa na sera mpya ya mifugo.

Ndaki, alibainisha hayo juzi jijini hapa wakati akizindua rasmi bodi ya TALIRI na kubainisha kuwa ni vigumu kuwa na sera bila kuwa na utafiti.

Kutokana na hali hiyo alisema TALIRI inapaswa kufanya utafiti kwa kuzingatia maelekezo, ubora na mahitaji ya wafugaji kwa kuwa mahitaji ni mengi na matatizo ni mengi yanayohitaji utatuzi.

Alisema, kwa vile serikali inaelekea kuwa na sera mpya ya mifugo, TALIRI inapaswa kushiriki kikamilifu ili kufahamu mwelekeo wa namna sekta ya mifugo inaweza kuendeshwa kwa kuzingatia hali halisi ya sasa.

"Kutokana na mabadiliko ya tabianchi, tukizingatia wingi wa shughuli za binadamu, mazingira ya sasa kwa namna ya masoko ya bidhaa za mifugo uzalishaji na biashara ya mifugo kwa ujumla, masuala ya namna hiyo lazima kwenye sera yatuelekeze namna ya kuendesha sekta ya mifugo." alisema Ndaki.

Mwenyekiti wa Bodi ya TALIRI, Prof. Sebastian Chenyambuga, alisema bodi hiyo itahakikisha inasimamia masuala ya utafiti kadri inavyotakiwa kwa kutoa matokeo ya namna ya kuendesha sekta ya mifugo na kutatua changamoto zilizopo.

Prof. Chenyambuga aliongeza kuwa bodi itaisimamia TALIRI kufanya utafiti wa masuala mbalimbali ambayo yamekuwa yakiibuka ghafla na mengine kusababisha taharuki kwa umma.

Awali, kabla ya bodi hiyo kuzinduliwa rasmi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, katika wizara hiyo anayesimamia sekta ya mifugo, Tixon Nzunda, aliwataka wajumbe wa bodi kuwa na mpango wa upatikanaji wa fedha ili kupata rasilimali fedha kwa ajili ya kufanya utafiti mbalimbali.

Pia alisema, bodi ni lazima ije na mpango wa mabadiliko ya taasisi ambao inalingana na mahitaji ya sasa ambao utashirikisha sekta binafsi wakiwamo wachakataji na wazalishaji wa viwandani.

Vilevile, aliitaka bodi hiyo kwenda kuisimamia taasisi ya TALIRI ili kuacha kufanya kazi zake kwa mazoea.

"Lazima msaidiane mkataba wa utendaji kazi muwape majukumu ya kufanya kwa muda wa mwaka mmoja kuona nini wamefanya ili waache kufanya 'business as usual (kazi kwa mazoea).

"Lakini nataka bodi hii iendea kuibadilisha NARCO katika utendaji wake wa kazi bado hakuna kilichofanyika ili kuleta tija kwenye sekta ya mifugo licha ya kuwa na mifugo mingi nchini" alisema Nzunda.





## Serikali yakiri kiwanda cha mafuta kiko hoi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Viwanda, Omar Said Shabani amesema takriban mwaka mmoja na nusu sasa uzalishaji wa mafuta kwenye kiwanda cha mafuta ya makonyo Pemba kinachomilikiwa na serikali kupitia Shirika la Biashara (ZSTC) siyo mzuri.

Alitaja sababu za uzalishaji wa kiwanda hicho kutokua mzuri ni kutokana na kuharibika kwa mitambo na vifaa vingine pamoja na tatizo la umeme kwenye kiwanda hicho.

Alibainisha hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Wawi, Bakari Hamad Bakari aliyetaka kujua hali ya uzalishaji wa kiwanda hicho.

Alisema kiwanda hicho huzalisha mafuta ya makonyo yatokanayo na karafuu na mafuta mengine ya mimea ikiwamo mafuta ya mkaratusi, mchaichai, mrehani na mdalasini.

Waziri huyo alisema jitihada mbalimbali zimechukuliwa na ZSTC ukiwamo ununuzi wa vifaa hivyo kutoka ndani na nje ya nchi lakini kiwanda hicho kimeshindwa kufanya uzalishaji kama ilivyotarajiwa na hivyo kusababisha shirika kuingia gharama kubwa za uendeshaji.

"Mheshimiwa Spika, baada ya kutafakari kwa kina juu ya gharama kubwa zinazokikabili kiwanda hicho, serikali imeliagiza shirika kuchukua hatua ya kukikodisha kiwanda hicho," alibainisha.

Alisema hadi sasa shirika limeiandikia barua Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kwa ajili ya kupata mwongozo wa namna litaweza kupata mwekezaji kwa lengo la kuongeza ufanisi pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji kwa shirika.

# Madaktari bingwa Uturuki kutoa matibabu Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

OFISA Uhusiano wa Hospitali ya Tasakhtaa Zanzibar, Victoria Mwakanjuki, amesema ujio wa madaktari bingwa kutoka Uturuki kutoa matibabu hospitalini huko, utaimarisha utoaji wa huduma za afya.

Akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake mjini Zanzibar kuhusu ujio wa madaktari hao, Victoria alisema hospitali hiyo imeingia makubaliano ya ushirikiano na madaktari bingwa wa Uturuki hasa kwa magonjwa ya moyo na mifupa.

Mwakanjuki alisema ushirikiano huo utasaidia kubadilishana ujuzi na uzoefu wa utoaji wa huduma ya maradhi hayo kati ya madaktari wa Hospitali ya Tasakhtaa na madaktari hao kutoka Uturuki.

Alisema lengo kuu la kuingia makubaliano na madaktari hao bingwa ni kuendelea kutoa matibabu bora katika hospitali yao.

"Madaktari hawa wametoka Uturuki kwa ajili ya kusaidia wazanzibar na hospitali yetu kutusaidia kupiga hatua katika utoaji wa huduma za afya kama walivyokuwa wao na imani yetu litafanikiwa," alisema.

Aliishukuru serikali kwa kuwasaidia katika hatua mbalimbali za kuwawezesha madaktari kutoka nchi mbalimbali kufika nchini kuwasaidia madaktari wazalendo huku akiupongeza uongozi wa hospitali hiyo kupitia mwenyekiti wake, Taufiq Salim Turk kwa kuleta madaktari kutoka nje ya nchi kwa lengo la kuwasaidia wananchi wa Zanzibar kupata matibabu.

Aliwataka wananchi kuitumia fursa hiyo ya madaktari hao bingwa kwa kuchunguza afya zao na watakaobainika kuwa na magonjwa ya moyo na mifupa, watapatiwa matibabu.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo kutoka Uturuki, Dk Adman Kaya, alisema wana uzoefu mkubwa wa kufanya upasuaji kwa wagonjwa wa moyo na huko kwao wana hospitali 24 zinazotoa huduma hiyo.

"Tupo Tanzania ambapo tutatoa huduma kwa Hospitali ya Tasakhtaa na pia tutaenda Dodoma kusaidia huduma za magonjwa ya moyo na mifupa," alisema.

Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani na Mifupa, Dk. Simion Bungusi Samuel na Dk. Benson Mwakalukwa wa Hospitali ya Tasakhtaa, walisema kwa kushirikiana na madktari bingwa wa Uturuki watafanya upasuaji hospitalini huko ili kuwapunguzia gharama ya kufuata matibabu nje ya Zanzibar.




Ofisa Uhusiano wa Hospitali ya Tasakhtaa Zanzibar, Victoria Mwakanjuki (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, ofisini kwake Mnazi Mmoja Zanzibar jana, kuhusu ujio wa madaktari bingwa kutoka nchini Uturuki, kwa ajili ya kutoa huduma ya matibabu hospitalini hapo. Kushoto ni Daktari wa Magonjwa ya moyo wa hospitali hiyo, Dk. Adman Kaya na Dk. Sami Sokoco kutoka Uturuki. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yatoa ufafanuzi ukodishaji wa visiwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, amekumbusha kuwa mwishoni mwa miaka ya 80 Serikali ya Zanzibar ilifungua milango katika sekta ya utalii kwa lengo la kukuza uchumi.

Alisema katika kufanikisha hilo kwenye miaka ya 2000 serikali iliruhusu ukodishwaji wa visiwa vya Mnemba, Chapwani, Changuu na Bawe ambapo kwa wakati huo mapato ya serikali katika ukodishwaji wa visiwa hivyo yalijikita zaidi katika kuangalia mapato yatokanayo na kodi ya ukodishwaji ardhi.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi huko Chukwani wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Pandani, Prof. Omar Fakihi Hamad aliyetaka kujua vipimo na muda wa majaribio uliotumika ukodishwaji wa visiwa 10 kati ya 53 vilivyopo Zanzibar.

Alisema visiwa hivyo vinne vilikodishwa kwa mkataba wa muda wa miaka 33 lakini baada ya kuingia madarakani, Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliagiza suala hilo lipitiwe upya na kuhusisha uamuzi wa ukodishwaji wa visiwa kwa madhumuni ya kutanua wigo wa uwekezaji katika sekta ya utalii kwa kufungua fursa zaidi za uwekezaji na uendelezaji wa matumizi mazuri ya rasilimali za bahari.

"Serikali iliamua kuruhusu uwekezaji katika visiwa hivyo ambapo jukumu hilo lilisimamiwa na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA)," alisema Soraga.

Waziri huyo alisema vipimo vilivyozingatiwa kwa wawekezaji hao ni uwezo wa mwekezaji katika kuhifadhi mazingira na kisiwa, uwezo wa mwekezaji kifedha, mikakati ya mwekezaji katika kuishirikisha jamii inayozunguka kisiwa na aina ya uwekezaji, kiwango cha mtaji kitakachowekezwa na malipo ya utangulizi kwa ajili ya ukodishwaji wa kisiwa.

"Mheshimiwa Spika, wawekezaji wote wamepatiwa masharti ya mkataba kama ilivyoelekezwa kwenye sheria ya matumizi ya ardhi ya mwaka1992," alisema.

Waziri Soraga alisema wawekezaji hao wamepewa muda wa miezi sita baada ya kukabidhiwa kisiwa wawe wameanza utelekezaji wa mradi.


Alisema serikali haijasita kukodisha visiwa vingine bali inaendelea kuvitangaza visiwa ambavyo vina mwonekano wa kuvutia wawekezaji kwa mujibu wa masharti yanayowekwa na serikali, hasa yale ya kulinda maslahi ya wananchi waishio karibu na visiwa hivyo na kulinda mazingira.

Alisema serikali baada ya kukodisha visiwa 10 vya mwanzo kwa ajili ya uwekezaji, imeendelea na mchakato wa kutangaza visiwa vingine 10 kwa uwekezaji ambapo visiwa saba kati ya hivyo vya awamu ya pili, tayari wameshapata wawekezaji na kufanya idadi ya visiwa vyote vilivyokodishwa hadi Septemba 2022 kufikia 17.

Alivitaja visiwa hivyo ni Bawe, Changuu, Kibandiko/Snake, Kwale, Pamunda A, Pamunda B, Chapwani, Pungume, Popo, Miwi na Niamembe Unguja na Njao, Matumbini, Kashani, Kwata, Mtangani na Misali Pemba.

Alisema matarajio ni kukusanya dola milioni 19.8 kama malipo ya awali na mtaji wa kiasi cha dola milioni 442.5.

"Hadi sasa malipo ya awali ya dola za Marekani milioni 11.1 yameshalipwa kwa baadhi ya visiwa vilivyokamilisha taratibu," alisema Soraga.



**JOKATE**

UKURASA 16

JUMAMOSI SEPTEMBA 24, 2022

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



# ZUCHU

## unataka kuvuruga wenzio

YUKO WAPI ?

# ABDALLAH HEMBA

## Pumzi ya farasi iliyosepa Sikinde




**Na Adam Fungamwango**

HIVI karibuni mwimbaji nguli wa bendi ya Mlimani Park, Orchestra, Abdallah Hemba alitangaza kuondoka, akidai kuwa mambo hayapo sawa kwenye uongozi.

Hata hivyo, kiongozi wa bendi hiyo, inayotumia mtindo wa Sikinde Ngoma ya Ukae, Habib Jeff, amesema kuondoka kwa mwanamuziki huyo kulitokana na kusimamishwa kufanya kazi katika moja ya shoo kwa kosa la uchelewaji na wala haikuwa kuwaondoa kwenye bendi bali kuwapa adhabu.

Hata hivyo, kauli ya kiongozi huyo haiondoi ukweli kuwa Hemba, ambaye hivi karibuni tu alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Muziki wa Dansi (CHAMUDATA), ameiacha bendi hiyo kongwe na sasa amejiunga na Sikinde Original.

Katika mahojiano maalum aliyoyafanya na BT, Hemba amesema awali haikuwa bendi kamili bali ilikuwa ni 'zing zong', yaani ni kundi ambalo wanamuziki wanakutana, wanarekodi na kurejea kwenye bendi zao.

"Ni kama wakati ule marehemu Tx Moshi Wiliam alivyokuwa na kundi la Bana Mwambe, huku akiwa ni mwanamuziki wa Msongo Ngoma. Lakini baada ya haya yaliyotokea, tumeamua sasa iwe bendi kamili," amesema mwanamuziki huyo.

Kutokana na kauli yake ina maana sasa kuna makundi mawili yanayofanana, na kugawana wasanii.

Kuna wanamuziki wamebaki Mlimani Park Orchestra, na wengine wamehama na Hema kwenda Sikinde Original.

Hii inakumbushia mwaka 1996, kundi hilo lilipogawanyika na baadhi ya wanamuziki kwenda kuunda kundi lingine lililoitwa Super Sikinde, ambalo hata hivyo halikudumu sana kwenye anga ya muziki.

"Nakumbuka hilo kundi hata mimi nilikuwemo, waimbaji tulikuwa watatu, Joseph Lusungu, Tino Masinge na mimi," anasema mwimbaji hiyo mwenye sauti nzito inayoshabihiana na ya Max Bushoke, Cosmas Chidumule na Muhidini Maalim Gurumo.

Bendi hiyo ilitishia uhai wa Sikinde Ngoma ya Ukae, baada ya kutoa wimbo uliokuwa na maneno yasemayo "kulamba asali kwa ncha ya kisu ni hatari, utamu ukikolea, utang'ata ulimi'

Baadaye huo ukawa ndiyo mtindo rasmi wa bendi iliyotikisa kwa muda mfupi.

Hemba, ambaye ni mwenyeji wa Kijiji cha Palala , Wilayani Kisarawe mkoani Pwani alisema kabla ya kujiunga na Sikinde alikuwa mwimbaji wa bendi ya Mchinga Sound.

"Nimepigia Mchinga Sound na kina Muumini Mwijuma na baada ya hapo, nikaenda DDC Mlimani Park 2004. Siku hiyo nilifika ukumbini kutembelea Sikinde, Shaaban Dede alikuwa ndiyo ameondoka kurejea Msondo, lakini alikuwa ameacha wimbo unaitwa 'Mama Kiwete', baadhi ya waimbaji walikuwa hawaweza kuuimba vizuri," ameeleza Hemba katika mazungumzo yake.

"Mpiga solo marehemu Kassim Rashid aliniona, akanifuata akaniambia nipande nikaimbe ule wimbo, ananifahamu sana na anajua naweza kuuimba, nikapanda na kuutendea haki. Nilipomaliza, Hassan Rehani Bitchuka alinifuata na kuniambia wananihitaji kwenye bendi." Ameongeza.

Anasema mwanamuziki huyo na ndiyo mwanzo na kukaa Sikinde kwa miaka 18 sasa, kabla ya kuondoka.

Faida ambayo ameipata kwenye muziki, mbali na kumfanya aendeshe maisha yake, ni kujulikana na watu wengi ndani na nje ya nchi, lakini pia kwenda mikoa karibuni yote ya Tanzania, na nje ya nchi hususan barani Ulaya.

"Kwa sasa tupo kwenye mazoezi makali ya bendi yangu hiyo mpya, hivi karibuni tutatoa nyimbo zetu, mimi mwenyewe binafsi nina nyimbo mbili ambazo nimezitunga. Bado sijazipa jina, lakini tunazifanyia mazoezi. Na siwezi kusema zinazungumzia nini kwa sababu siku hizi zama za sayansi na teknolojia, pia watu wamekuwa hawajitumi na wavivu, wakisoma tu maudhui ya wimbo wa mtu Fulani, wao wanachukua haraka na kuyafanyia kazi, hili limekuwa tatizo sana, na ndiyo maana unaona hata watu wa bongo fleva tunasikia wanalalamikiana kuibiana nyimbo," Akabainisha mwimbaji huyo.

# UDAKU TU



## Kisa wafuasi mil 10, wema ashambuliwa

UJUMBE wa msanii mkongwe wa filamu, Wema Sepetu, ambao aliuandika kwa ajili ya kuwashukuru mashabiki zake kwa kufikisha wafuasi milioni 10 katika mtandao wa Instagram, umesababisha taharuki.

Katika ujumbe huo aliouweka katika ukurasa wake wa Instangram, Wema kutokana na idadi hiyo, kamwe wasimfananishe na msanii yeyote wa kike kwa sababu hakuwahi kuwa katika mashindano yeyote.

"Basi naombeni kuanzia sasa, Msinishindanishe na mtu jamani, Sijawahi kuwa katika mashindano zaidi ya Miss Tanzania 2006," ilisema ujumbe huo.

Hata hivyo, baadhi ya mashabiki walimjia juu kwa kumjibu kwamba ana hofu na Hamisa Mobeto, ambaye kila kukicha anaongeza idadi ya wafuasi ambao kwa sasa amefikisha milioni 9.9.

**bry_nuckle** ameandika "Zama zako zimepita Kisa unamuona @ hamisamobetto yupo na 9.9 Unaanza uswahili kwani hujiulizi ulikuwa unamzidi tofauti ya milioni 2, ukowapi kubali matokeo,"

**officialwemasepetufans** ameandika "Achana nao hao hata kwenye shida wao wanataka kuongelewa kwa ajili ya maslahi yao binafsi,"

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**IRINE UWOYA**
@ireneuwoya8
"Maisha imekuwa ndefu sana acha mzungu afupishe aite life.....na life oooh"



**ZUCHU**
@officialzuchu
"Mwanamke wa 1 afrika mashariki kufikia hatua hii,mwanamke wa pili afrika nzima na wa 4 Afrika Mashariki, mwanamke pekee katika 4 bora. Asanteni sana



**BATULI**
@batuliactresstz
"Kilinde Alichokupa MWENYEZI MUNGU, Wengi Wanakiomba Na Hawajapewa,"



**NANDY**
@officialnandy
"Sio kwamba napenda kuwa king'ang'anizi tatizo mazoea...Mungu aliumba mapenzi lakini yana watu wake."



**SHAMSA FORD**
@shamsaford "Tangu nimetoka kwenye ndoa ni miaka 3 sasa. Nimejipa muda wa kutosha na kupata elimu kubwa juu ya mahusiano.Sasa hivi akili yangu imetulia nipo tayari kuolewa tena, Inshaaallah.. .Sitaki kuendelea kufanya zinaa mimi ni binadamu sijui mwisho wangu ni upi. Inshaaallah Mwenyezi Mungu unipe mume mwenye kheri na mimi atayenipenda,"

BASI SAWA

## Lukamba: WCB kuna wenye roho za kimaskini



ALIYEKUWA mpiga picha wa lebo ya Wasafi (WCB), Lukamba, amesema roho za kimasikini zinawasumbua baadhi ya watu wanaomzunguka Diamond Platnumz, kiasi cha kutamani kuona anakwama kimaisha.

Lukamba amesema, hakuna mtu anayeweza kumfahamu vizuri Diamond, lakini kumeibuka watu walioingia sasa katika lebo hiyo wana kazi ya kumzungumzia kana kwamba wanajua kila kitu.

"Nyie mmekuja tu tafuteni liziki zenu, sawa mimi nimeondoka wasafi, lakini kunizungumzia ni chuki inayotengenezwa. Mimi nimetoka kwa mambo yangu, nina furaha na amani yangu ya moyo kuondoka lakini wapo wenye roho ya kimasikini wanatamani niwe mtaani nalia njaa," amesema Lukamba.

## Manfongo alia 'Mtoto Ameharibika'




MKALI wa muziki wa Singeli, Manfongo, ametambulisha kibao kipya 'Mtoto Ameharibika' alichokipakua akishirikiana na mkongwe Mr Blue.

Akizungumza na BT, Manfongo amesema ngoma hiyo ni mfululizo wa kazi zake ambazo anaamini kwa ajili ya kukidhi kiu ya mashabiki wake wa ndani na nje ya Tanzania.

"Mtoto Ameharibika ni ngoma ambayo ipo katika mpango wangu wa kwenda kimataifa, Mr Blue ameshiriki kikamilifu kuhakikisha ladha inakuwa tofauti na inayokidhi kiu ya mashabiki zangu," amesema manfongo.






## UJUMBE WA JOKATE WAIBUA UTATA

MKUU wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo ambaye pia anajihusisha na mitindo, ameibua mjadala katika mitandao ya kijamii baada ya kuweka picha yake ya utotoni huku akiambatanisha na ujumbe mzito.

Katika ukurasa wake wa Instagram, Jokate aliweka pichi hiyo huku akinogesha na ujumbe unaosema "Sisi ndio wale tunaosaidiwa na Mungu, kuanzia kuzaliwa kwetu mpaka hapa tulipo ni nguvu na uweza wake Mungu. Ameeeen"

Baadhi ya watu waliochangia ujumbe wake walionekana kuwa njia panda huku wengine wakimpongeza na baadhi walitaka ufafanuzi kuhusu anachomaanisha.



## Zuchu unataka kuvuruga wenzio

MWANAMUZIKI nyota wa Bongo Fleva, Zuchu, ameibua bifu jipya kwa wasanii wenzake wa kike baada ya hivi karibuni kueleza hawezi tena kushindana nao na badala yake anataka kushindana na wasanii wa kiume.

Kauli hiyo ambayo inadaiwa kama inamlenga mshindani wake wa karibu Nandy, imeleta mtafaruku kiasi ambacho baadhi ya watu wamesema imeongeza chuki kwa wasanii wenzake wa kike.

Hivi karibuni Zuchu kupitia ukurasa wake wa Instagram, aliandika "niwashukuru wazazi wangu ni kwa ajili yenu na uwezo wa M/Mungu tu. kwa uandishi wangu yafaa kuwekwa kwenye ligi za wanaume wadada wenzangu ntawaonea tu,"

## TWISTI 5 ZILIZOCHENGUA WABONGO

**Na Adam Fungamwango**

MUZIKI una safari ndefu sana. Miaka ya 1950 hadi mwanzoni mwa miaka ya 1970 kulikuwa na wanamuziki waliovuma sana Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Wanamuziki nao ni kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Zambia, Tanzania, Kenya na Uganda. Nitawaelezea wiki ijayo, lakini ngoja leo nitaje majina yao.

Hao ni Daudi Kabaka, Losta Abelo, Edward Masengo, Charles Sonko na dada yake Frida Sonko, Nashil Pichen, Peter Tsosi, John Zenze, Fadhili William na wengine wengi ambao wiki ijayo nitaweka historia zao hapa.

Hawa licha ya kuwa wametoka kwenye nchi mbalimbali na hakuna Mbongo hata mmoja, lakini walikuwa maarufu sana hapa nchini kutokana na nyimbo zao kukubalika kwa kiasi kikubwa. Moja ya staili ambazo zilipendwa sana Kenya na hapa Bongo ni 'twist'. Hadi leo kwenye sherehe za harusi, wazee huwekewa nyimbo za 'twisti' ili kujikumbusha wakati wa ujana wao.

Ni uchezaji unaoleta burudani ya aina yake ya kusugua miguu, huku mwili ukienda chini, upande mmoja, halafu unabadilisha upande mwingine. Wakati mwingine unarusha hata mguu mmoja wakati wa kubadilisha staili ya uchezaji wa 'twisti'.

Mwanzilishi wa aina hii ya uchezaji ni Mmarekani Chubby Checker, jina lake halisi ni Ernest Evance, aliyezaliwa Oktoba 3 na ikifika tarehe hiyo mwaka huu, atakuwa anafikisha umri wa miaka 81. Yupo hai hadi leo.

Afrika Mashariki hasa Kenya, Kabaka, ndiye alionekana kuwa mtaalam wa muziki huo, hivyo kurekodi nyimbo nyingi zilizovuma sana hadi kuchengua Wabongo wengi. Hizi ni baadhi ya nyimbo maarufu za 'twisti' nchini.

**Tanganyika Twisti-Daudi Kabaka**

Ni wimbo ambao Kabaka anamwimbia mpenzi wake Masita, kuwa anakwenda safari Tanganyika. ( Tanzania kabla ya Uhuri mwaka 1961)

Inavyoonekana mpenzi wake ana wasiwasi, lakini jamaa anamtuliza na kumwambia hawezi kumpenda msichana mwingine yeyote zaidi ya yeye.

Anamwambia aliwahi kufika huko, akatokea msichana akampenda lakini kila anachofanya anamkumbuka Masita, wake yuko Nairobi, hiyo inaonyesaha upendo wake mkubwa wake na hawezi kumsaliti.

**Angelike-John Zenze**

Ni wimbo wa mapenzi, jamaa anamlilia Angelike, mpenzi wake ambaye wamegombana na kuhitilafiana.

Anamwambia arudi waoane, roho yake kila siku inamsumbua. Anakumbuka mengi walivyokuwa wakifanya wakati wa kilele cha penzi lao, hivyo warudiane na wasahau yaliyopita.

**Msichana wa Elimu-Daudi Kabaka**

"Msichana wa sura nzuri ni kitu gani kinachokufanya usiolewe, elimu unayo ya kutosha, hata ng'ambo ukaenda ukarudi.

Msichana wa urembo kama wewe uonyeshe mapenzi kwa vijana, ukileta dharau kwa wanaume utazeeka ukiwa nyumbani kwenu, ona watoto wa nyuma yako, wameolewa wamekuacha ukihangaika."

Haya yote ni maneno yaliyomo kwenye wimbo huo. Unawaasa wanawake hasa wenye elimu kubwa ambao wana tabia ya kuona wao ndiyo kila kitu na kuwadharau baadhi ya wanaume, matokeo yake wanaogopwa na kukwepa dharau, hivyo kukosa wapenzi.

**Taxi Driver-Fadhili William**

Jamaa anamtaka dereva taxi aendeshe gari kwa haraka kwenda Nakuru akamuone mpenzi wake Anna, aliyemuandikia barua afike Jumamosi. Lakini gari lilipofika Naivasha gari lilipata pancha. Ikawa sasa lazima wachelewe. Alipofika Nakuru alimkuta mpenzi wake amekasirika, ikabidi amwambie ukweli kuwa halikuwa kosa lake, ila gari lilipata pacha.

**African Twisti-Daudi Kabaka**

Huu ni wimbo wa ajabu kidogo. Umetengenezwa enzi ya uduni wa teknolojia, lakini ikawezekana kubadilishwa sauti za binadamu kuwa kama wanaoimba ni wanyama.

"Afrika wote wanapenda twisti, hata sisi wanyama na mwituni tunaipenda na kuimba.

Tucheze tuimbe twist sisi wanyama wa mwituni." Sauti ni kama za vikatuni, lakini nikipangiliwa kwa sauti.

Wanyama hao ni kindi, ambao mmoja aliimba sauti ya kwanza ni Zangu, na yule aliyeimba sauti ya tatu na ya pili ni Juma.

FILAMU

## Nikita: Penzi haligawanyiki

**Na Adam Fungamwango**

DUNIA inagawanyika, mali na shamba vinagawanyika, lakini siyo penzi, litafanya kila njia upande mmoja litazidi. Haya ni maneno ambayo yamo kwenye wimbo wa Vijana Jazz uitwao 'Penzi Haligawanyiki.'

Na upo mwimbo mmoja wa taarabu ya zamani ambao unaimbwa 'itakuwaje kutupenda wawili, hali ya wewe una moyo mmoja. Najua utadanganya mmoja, kama yeye kama mimi sijui.'

Ni kwamba wanamuziki, wasanii na kila mmoja anayepitia mapenzi, ameshagundua kuwa binadamu kwa sababu ana moyo mmoja, basi atapenda mmoja tu. Mwanaume hata akiletewa wanawake mia, atatamani wote, lakini baada ya muda atajikuta anampenda mmoja tu kati ya wote. Na kila mtu atajua anayependwa zaidi ni nani. Hata mwanamke pia ni hivyo hivyo. Hata ujibaraguze na kubadilika, lakini mwili utakuwa na huyu, lakini moyo utabaki kumpenda yule yule.

mambo ni mengi, muda ni mchache. hebu tuangalie hili kwenye filamu iitwayo 'Nikita'.

Imechezwa na Swalehe Omari, Rehema Shaaban, Ally Bwijo, Omega Emmanuel, Sebastian Madeko, Fatuma Ally, Neema Ngoi na wengineo.

Picha linaanza kwa Stanley kijana anayesoma Uingereza, anarejea nchini na kukutana na kimwana Nikita akatokea kumpenda.

Hata hivyo, msichana huyo ana mpenzi wake Jeff, ambaye ametokea kumpenda. Anashindwa kumpenda mwingine, anamwambia kuwa ana mpenzi, hivyo hawezi kuwa naye.

Mama Stanley, anataka kijana wake aoe. Na ana rafiki yake ana msichana ambaye wamepanga waoane. Kinachokwenda kutokea ni kwamba Stanley alipofika huko na mama yake walikutana na Nikita. Kumbe mama wa Stanley na Nikita wanafahamiaka kitambo.

Kitendo cha Nikita kumkataa Stanley kwa sababu ya Jeff kilimkasirisha mama yake, kwani kijana huyo ni fukara, binti yake akiwa msomi na kumkataa kijana msomi mwenzake.

Tukio la kukataliwa mpenzi wake na kumfukuzwa kama mbwa nyumbani kwao lilimsononesha Nikita, na kuamua kubadili mawazo ili aolewe na Stanley. Akavishwa pete, huku matayarisho ya harusi yakifanyika.

Wakati huo huo, Jeff ambaye aliachwa mpweke, akili yake ikajikita zaidi kwenye usanii kwani alikuwa mwimbaji mzuri, kwa bahati mbaya alikuwa 'hajatoka'.

Wimbo wake aliourekodi ulianza 'kuhiti' na kuanza kuwa supa staa. Tukio la kumuona kwenye televisheni akiwa staa lilimshtua Nikita, akapatwa



mshtuko wa moyo akalazwa hospitalini. Ilikuwa ni aibu kwa Stanley na ndugu zake.

Daktari anawaambia bila kwenda Jeff, binti huyo hatopona. Mama anamfuata Jeff nyumbani kwake na kumhadithia jinsi ilivyotokea.

Jeff, pamoja na kunyanyaswa, moyoni alikuwa anampenda sana alikubali kwenda hospitalini. Akafika na kumkuta hoi. Jeff akamwambia anampenda na hataki kumpoteza, Nikita akapata nafuu. Kumbe hata yeye nafsini mwake alimpenda Jeff, tatizo ilikuwa ufukara tu.

# BARIZI LA PWANI

# Nani wa kulaumiwa kuanguka kwa taarab?



**Na Mwandishi Wetu**

HIVI karibuni kulifanyika tamasha la aina yake la muziki wa taarab katika ukumbi wa Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam.

Katika shoo hiyo ambayo iliwakonga nyoyo mashabiki wa muziki huo, wakongwe watatu wa muziki huo Khadija Kopa, Sabah Salum na Leyla Rashid, walipanda jukwaani na kila mmoja alionekana kuimba kwa ustadi wa hali ya juu.

Tamasha hilo ambalo lilikuwa likirushwa moja kwa moja na kituo cha TV, lilionekana kama alama ya muziki huo kurejea tena katika ubora wake kama ilivyokuwa miaka ya 2000 ambako taarab ulikuwa moja ya muziki pendwa kwa kila rika.

Kila mwimbaji aliyepanda jukwaani alionekana kufanya vyema na kusababisha watu walioingia kutokaa katika viti vyao, wakati wote walinyanyuka na kucheza.

Hata hivyo, baadhi ya wadau wa muziki huo, wamesema tamasha hilo limeonyesha jinsi gani Muziki wa taarab unavyokubalika katika jamii, lakini umeporomoka kutokana na wasanii wenyewe kuingiza mambo ambayo hayakubaliki.

Abdallah Kusi, amesema kwamba kuchanganywa kwa maadhi ya taarab ile ya asili na ule wa kisasa imesababisha muziki huo kukosa mwelekeo, na kisha kushuhudia ukianguka kwa kasi.

Ameeleza kwamba, ushahidi unaonekana wazi jinsi nyimbo za zamani zinavyoonekana kupendwa hadi sasa, tofauti na zile zilizotoka miaka ya hivi karibuni.

"Muziki wa taarab walioua wasanii wenyewe kwa kuingiza usasa na kusahau miiko ya muziki, sasa wanatakiwa kujitathmini kama wanahitaji kuufufua na kuwa pendwa kama zamani," amesema Kusi.

Amesema, kulingana na mwitikio wa mashabiki katika tamasha hilo la Taarab, bado muziki huo upo katika mioyo ya watu, lakini hakuna watu wa kuunyayua tena kwa kuwekeza kama ilivyo kwa Bongo Fleva.

"Ni lazima watu waanze kuwekeza katika muziki huu kama ulivyo Bongo Fleva, redio na vituo vya televisheni watenge muda wa kupiga nyimbo kama ilivyokuwa zamani na ninaamini kila kitu kitakuwa sawa," ameongeza kusema.



# BATA LA WIKI

Je una kiwanja cha burudani piga -0717336368

**Twanga Pepeta**
Kila Ijumaa wapo Mawasiliano Park Ubungo, Jumamosi ndani ya ukumbi wa Andrews Lounge Sinza na Jumapili wanawasha moto, katika ukumbi wa Gwambina Lounge Chang'ombe.

**Waluguru Original**
Makao yake yapo mjini Morogoro, hutoa burudani kuanzia Alhamisi katika ukumbi wa Didi's Break Point Iringa Road, Ijumaa ndani ya ukumbi wa Kambarage SUA, Jumamosi Terminal Pub Msamvu na Jumapili wapo F2 Florida.

**Kimokimo Band**
Bendi hii ambayo inaongozwa na mwimbaji wa siku nyingi Khadija Kimobitel, hutoa burudani siku mbili kwa wiki ambapo Ijumaa wapo Kontena Kibaha mkoani Pwani na Jumamosi, katika ukumbi wa Kijichi Royal Garden Dar.

**The Kilimanjaro Band**
Wanapenda kuitwa 'Wana Njenje', ambao Jumamosi hii watafanya onyesho katika ukumbi wa Golden Rose BBQ jijini Dodoma, ikiwa ni mara kwanza tangu bendi hiyo ilipoanzisha miaka 48 iliopita na pia ni mara ya kwanza tangu kufiwa na mpiga kinanda wao Waziri Ally, Julai mwaka jana.

**Mambo Live Band**
Kila Ijumaa inafanya vitu vyake katika ukumbi wa The Crown Pub, kisha Jumamosi inakuwa ndani ya ukumbi wa Village Hotel.

**Msongo Ngoma**
Ijumaa wanatoa burudani katika ukumbi wa Gwambina Lounge Chang'ombe, Jumamosi wapo Makutano Park Vikindu mkoani Pwani na Jumapili wanakuwa ukumbi wa Dar Safari Buza Dar.

**Maina Band**
Wao huanza kutoa burudani siku ya Alhamisi, katika ukumbi wa The Marz, Namanga, Ijumaa wapo Regancy Park, Jumamosi External na Jumapili wanamalizia wikiendi ndani ya ukumbi wa Trinity Oysterbay.

**Bogos Musica**
Chini ya Nyoshi El-sadat, ijumaa huwa inatoa burudani katika ukumbi wa Masai Bar Mwananyamala, Jumamosi ipo ndani ya ukumbi wa Muungano Park ,kivule na Jumapili itakuwa Board Room Sinza Mori.

**Tukuyu Sound**
Kila Ijumaa wapo ukumbi wa TTG Kimara Korogwe, Jumamosi huwa wapo ukumbi wa Mikocheni na Jumapili wanamalizia wikiendi yao katika ukumbi wa Mawasialiano Park Ubungo.

BIRTHDAY TOTO
BURUDANI

# PRIYANKA
## ATIMIZA MIAKA 4

Happy Brithday

















BT BURUDANI TELE

TUMA PICHA BIRTHDAY TOTO
0717 336 368



# Levine akana kuwa na mchepuko

KIONGOZI wa kundi la Maroon 5, Adam Levine amekana kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Summer Stroh.

Katika chapisho lake katika ukurasa wa Instagram, mwimbaji huyo alikanusha penzi hilo na kueleza yupo imara katika ndoa yake.

"Nilitumia uamuzi mbaya katika kuzungumza na mtu mwingine yeyote isipokuwa mke wangu kwa namna yoyote ya kutaniana. Sikuwa na mchumba, hata hivyo, nilivuka mipaka katika kipindi cha majuto cha maisha yangu," aliandika.



## Dj Cuppy awashtukia wapenda kitonga

DJ maarufu wa Nigeria, Florence Otedola, maarufu kama DJ Cuppy ameeleza kuwa wanaume wengi wanajilengesha kwake kwa lengo la kujitajirisha.

Amesema, wanaume wengi aliokuwa na uhusiano wa kimapenzi anaamua kuachana nao baada ya kuonekana kutaka kuwa karibu na baba yake ambaye ni bilionea nchini humo.

"Nimerudi nyumbani nahisi kama wavulana wengi hawanitaki, wanamtaka baba yangu ambaye ni tajiri.

Nilichumbiana na mvulana mmoja siku moja aliniuliza lini atakutana na baba yangu, hapo niliamua kumbwaga," amesema.

## Kiddwaya yani huna wa kumwagilia moyo?

ALIYEKUWA mshirika wa shindano la Big Brother Nigeria, Kiddwaya amesema bado hajafanya maamuzi ya kuoa wala kumchumbia mwanamke.

Hivi majuzi, nyota huyo wa televisheni alidaiwa kumvisha pete ya uchumba mwanamke ambaye bado hajafahamika, licha ya kuonekana akivinjari naye katika mitaa ya maraha.

"Sijaoa na sina mchumba. Ilikuwa nafurahi kuona watu wanatoa majibu yote," amesema Kiddwaya.





## Polisi wapata viashiria kifo cha PnB

POLISI nchini Marekani, wanaumiza kichwa kuwabaini watu waliomuua rapa maarufu PnB Rock, huku kuna uvumi kwamba huenda watu waliofanya mauaji wanaweza kufahamiana.

Katika maoni ya awali ya polisi inaeleza kuna viashiria kwamba inaweza kuwa mauaji yaliyopangwa na adui ambaye anafahamika.

Vyanzo vinaeleza kwamba, wapelelezi wamepata viashiria hivyo kwa kuchunguza maisha yake binafsi na hasa akiwa katika mji wa Atlanta.

## Rita usichukie, yote ni neema

MWIGIZAJI nyota kutoka Nollywood Rita Dominic, amekanusha taarifa zilizosambaa mitandaoni kwamba amejifungua watoto mapacha.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter, Rita amesema kuwa kuna ripoti kadhaa kwenye mitandao ya kijamii kwamba amepata watoto mapacha na mume wake, Fidelis Anosike, jambo ambalo sio kweli.

Uvumi huo unakuja miezi kadhaa baada ya mwigizaji huyo kufunga harusi iliyojaa nyota mbalimbali.



MAKALA

# Almasi kubwa Afrika iliyopamba taji pekee la Malkia Elizabeth II

**Na Mwandishi Wetu**



JIWE kubwa zaidi la almasi katika taji la Malkia lenye thamani ya juu nchini Uingereza ndilo hazina ya kipekee iliyomilikiwa na Malkia Elizabeth II.

Inaweza kuelezwa kuwa almasi hiyo ilitokana na vipande vya kale vya sakafu ya bahari, ambayo ilibebwa na mkondo wa maji hadi chini ya sayari yetu na kisha kurudi juu tena.

Wakala wa mauzo ya madini katikati mwa London alipopima jiwe hilo lilikuwa na uzito wa zaidi ya pauni moja sawa na gramu 500.

Kumbukumbu inaeleza kwamba ilikuwa Aprili 1905, ikiwa miezi mitatu nyuma, Meneja katika mgodi wa Premier nchini Afrika Kusini alikuwa akikamilisha ukaguzi wa kawaida katika mgodi uliokwenda chini ya futi 18 chini ya ardhi, wakati huo alikuwa akitazama mwanga ulioakisiwa kwenye ukuta mbovu juu yake.

Alidhani ni kipande kikubwa cha glasi kilichochongwa na wenzake, kama mzaha alitoa kisu chake cha mfukoni na baada ya kuchimba, kisu kikachomoa mara moja jiwe linalong'aa.

Hatimaye mwamba huo uliondolewa kwa mafanikio, na kuonesha kuwa ni almasi halisi jiwe kubwa la karati 3,106.75, ikiwa karibu na ukubwa wa ngumi.

Haikuwa kubwa tu, lakini uangavu wake ulikuwa sio wa kawaida.

Cullinan, kama ilivyojulikana, ni almasi kubwa zaidi kuwahi kupatikana wakati huo.

Mara ilipong'arishwa na kung'olewa katika mawe kadhaa yanayoweza kudhibitiwa, kioo kikubwa zaidi ambacho kilitoa mng'ao wa nyota katika mfumo wa nyota ya mbali. Kwa hiyo, jiwe hili liliitwa Cullinan wakati mwingine hujulikana kama Nyota Kuu ya Afrika.

Karibu miaka 120 baadaye, almasi hiyo kubwa zaidi haijasahaulika.

Wakati wa msafara wa mazishi wa marehemu Malkia Elizabeth II, vizazi kadhaa vya Cullinan viliwekwa kwenye jeneza la Malkia, na zilitembea pamoja naye na kuondolewa wakati jeneza lilipokuwa likishushwa kwenye chumba cha kifalme kwa mazishi.

Hiyo ni kwa sababu leo hii jiwe hilo kubwa la thamani ni sehemu ya vito vilivyopo katika Taji hilo la kifalme, ambavyo kwa kawaida huwekwa katika jumba la makumbusho la taji la vito na hutolewa nje kwa matukio ya serikali.

Cullinan sasa inakaa katika Fimbo ya Mfalme wa Uingereza, wakati ndugu yake wa pili, Cullinan II, imepachikwa katika taji la kifalme lenye vito vya thamani. Hata hivyo, kabla almasi chafu haijaweza kubadilishwa na kuchukua nafasi yake katika historia, ilihitaji kuuzwa na London ilichaguliwa kama sehemu nzuri zaidi ya kufanya hilo.

Hapo ililileta tatizo kutokana na wasiwasi kwamba wanawezaje kusafirisha jiwe la thamani kama hilo maili 7,926 sawa na km 12,755, bila kuibiwa?

Mwishowe, jiwe hilo la thamani lilitumwa kutoka Johannesburg na posta ya kawaida, kwa gharama ya shilingi tatu pekee au kama Senti 75 za Marekani wakati huo.



Wakati huo huo, mfano wa almasi ambayo haikuwa halisi ilisafirishwa kwa safari ndefu kutoka Afrika Kusini hadi Uingereza kwa boti ya mvuke iliwekwa waziwazi sehemu salama ya nahodha na ililindwa na polisi wapelelezi kama mapambo tu.

Katika jambo la kushangaza, zote zilifanikiwa kufika. Baada ya miaka mingi ya kushindwa kuuzwa, almasi halisi iliyosafirishwa kwa posta ya kawaida, wakati huo ilinunuliwa na serikali ya Transvaal kwa paundi 150,000 sawa na dola milioni 5 za sasa, kisha alipewa zawadi Mfalme Edward VII.

Ingawa inajulikana ulimwenguni kote kwa ukubwa na uangavu, sifa hizi sio ajali, kwani Cullinan ilikuwa almasi ya "Clippir" ambayo ni jamii ya madini ya kipekee na ya kung'aa zaidi kuwahi kupatikana.

Pamoja na uzuri wote, almasi ni vipande vya ndani zaidi katika Dunia na vitu visivyo vya kwaida vya kijiolojia vinavyovutia ambavyo vimefichwa kama vito.

Madini haya hutokana na miamba ya ajabu kutoka eneo la ajabu lisiloweza kueleweka, lililozungukwa na miamba ya kijani kibichi na madini ambayo hayapatikani, chini kabisa ya uso wa Dunia.

Wanasayansi ulimwenguni kote wamekuwa wakitafiti kwa miongo kadhaa ili kufichua siri za eneo hilo na cha kushangaza, ni almasi ambazo zinaonekana.

**FURSA ISIYO YA KAWAIDA**

Akiwa ameketi mbele ya darubini katika Taasisi ya Gemological ya Marekani (GIA) mwaka 2020, Evan Smith alinyoosha glavu za mpira juu ya vidole vyake kwa uangalifu, na kuchungulia kwenye lenzi za kifaa.

Chini yake kulikuwa na almasi yenye karati 124 yenye uzuri wa ajabu.

Kufikia hatua hiyo, Smith alikuwa tayari amepitia karibu viwango vingi vya usalama vya kijeshi, ukaguzi wa Isis scans na utambulisho. Pia alipita katika milango kadhaa yenye udhibiti, lifti zenye usalama na vikwazo vigumu.

Wakati akifanya kazi, kamera za video zilionesha vizuri muonekano wa chumba na kufuatiliwa kwa karibu na walinzi waaminifu.

Smith mwanasayansi mkuu wa utafiti katika idara ya GIA - alikuwa akichunguza almasi kwa ujumla, jinsi kioo cha almasi kinavyoundwa na chini ya hali gani itakavyoonekana.

Hata hivyo, kufanya kazi ya almasi za thamani ya juu ni biashara ngumu kama anavyosema Maya Kopylova, profesa wa uchunguzi wa madini katika Chuo Kikuu cha British Columbia.

Anasema kupata sampuli za almasi yoyote ni ngumu, na nyingi anazofanya kazi zingeweza kutupwa.

"Watafiti wanapaswa kuwa na uhusiano mzuri na makampuni na kamwe hawatakupa sampuli muhimu," anasema.

"Kwa hivyo, hawataweza kutupatia almasi ambazo zina ukubwa wa 6mm sawa na inchi 0.2 au kubwa zaidi." Alichogundua Smith kilikuwa cha mapinduzi. Takriban robo tatu ya almasi ya Clippir ilikuwa na mifuko midogo midogo, au mipako ya chuma ambayo iliepuka kutu sio kitu ambacho ungepata katika almasi za kawaida ambazo zingine zilizobaki zilikuwa na aina ya garnet ambayo safu msingi ya juu huyeyuka.

Kwa utafiti wake wa 2020 pamoja na Wuyi Wang, ambaye ni makamu wa rais wa utafiti na maendeleo huko GIA, - Smith alichambua almasi ya karati 124 na kugundua kuwa iliundwa kwenye mwisho wa kina wa safu inayowezekana angalau kilomita 660 sawa na maili 410 chini ya uso wa dunia.

# Mzozo mashariki mwa DRC, unaokosa majibu ya suluhu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron, amechukua jukumu zito la kujaribu kutatua mgogoro unaotishia kuibuka kwa vita kamili kati ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Rwanda.

Kwa miezi kadhaa pande hizo mbili zimekuwa zikishtumiana kufadhili vikundi vya waasi walio mashariki mwa DRC.

Hata hivyo, DRC ndiyo inayolaumu zaidi kufuatia kuibuka upya kwa kundi la waasi la M23, ambalo linadhibiti baadhi ya maeneo ya Mashariki mwa nchi hiyo, huku ikiishutumu Rwanda kuwa nyuma yao.

Rais wa DRC, Felix Tshisekedi wiki hii katika hotuba yake katika Hadhara Kuu ya Umoja wa Mataifa, amelituhumu kundi la waasi wa M23 kuwalinganisha watu nchini mwake, na kuungwa mkono na Rwanda.

Mbele ya jukwaa hilo lililohudhuriwa na viongozi wa mataifa mbalimbali duniani,

Tshisekedi alisema, kuhusika kwa Rwanda katika mikasa inayopitia nchi na wananchi wake katika maeneo yanayokaliwa na jeshi la Rwanda na washirika wake M23, sio suala lenye shaka tena liko wazi.

Madai hayo sio mapya, kwani msuguano kati ya nchi hizo mbili kuhusu oparesheni za waasi wa M23 hutokea mara kwa mara.

Kundi hilo la waasi limekuwa kimya kwa miaka kadhaa lakini katika miezi ya hivi karibuni limeanza tena kufanya hujuma mashariki mwa DRC.

M23 imeongeza maradufu oparesheni zake katika maeneo ya mashariki mwa nchi hiyo karibu na mpaka wa Rwanda. Mnamo mwezi Juni, iliuteka mji wa kimkakati wa Bunagana karibu na mpaka wa Uganda.

Tshisekedi, ametahadharisha viongozi wa dunia kuwa, kushindwa kwao kwa namna yoyote ile katika kuzingatia ripoti za wataalamu wa Umoja wa Mataifa kuhusu mgogoro huo, huenda ukaichochea Rwanda kuendeleza uchokozi wake, na kufanya uhalifu wa kivita na uhalifu dhidi ya binadamu nchini mwake.

Kusuasua kwa viongozi hao wa dunia pia kutaongeza nguvu madai ya Wakongomani juu ya hatua ya Umoja wa Mataifa kuegemea upande mmoja, katika kile Tshisekedi alichokiita kushiriki kwa baadhi ya wanachama wa Umoja huo katika uhalifu unaofanyika.



Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Felix Tshisekedi na Rais wa Rwanda, Paul Kagame

**KAGAME AKANUSHA KUUNGA MKONO M23**

Hata hivyo, Rais wa Rwanda Paul Kagame, katika hotuba yake kwenye Hadhara hiyo, licha ya kuugusia mzozo wa mashariki mwa Kongo lakini alijizuia kumjibu Tshisekedi moja kwa moja.

Kagame, amekanusha mara kwa mara kuwa analiunga mkono kundi la waasi la M23. Rais huyo wa Rwanda aliendelea kueleza kuwa mzozo wa mashariki mwa DRC umeendelea kwa zaidi ya miongo miwili na kwamba unahitaji kutazamwa kwa jicho la karibu.

"Kupelekwa kwa kikosi cha walinda amani wa Umoja wa Mataifa kumewaweka majirani wa DRC katika hatari pia ya kushambuliwa. Kuna haja ya kutafutia suluhu ya haraka mzozo huo ili kushughulikia kiini cha ukosefu wa utulivu mashariki mwa DRC. Mchezo wa kutupiana lawama hautatui tatizo hilo." Amesema Kagame katika mkutano huo.

**GUTERRES AKIRI HALI NGUMU**

Tshisekedi na Kagame walikuwa wakizungumza siku chache baada ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres kukiri kwamba walinda amani wa MONUSCO hawana uwezo tena wa kukabiliana na waasi wa M23.

Guterres aliviambia vyombo vya habari vya nchini Ufaransa kuwa, Umoja wa Mataifa hauna uwezo wa kulishinda kundi la M23, akisema kuwa wapiganaji wa kundi hilo wana silaha za kisasa na za hali ya juu tofauti na wale wa MONUSCO.



Wapiganaji wa kundi la waasi la M23 wakiwa katika eneo wanaloshikilia mashariki mwa DRC.

Kauli ya Guterres iliwashangaza wengi na hata kukosolewa na baadhi ya wanaharakati nchini humo.

Mamlaka nchini DRC imetilia mashaka umuhimu wa walinda amani nchini humo.

Tangu mwaka 2019, kumezuka maandamano ya kushinikiza kikosi hicho kuondoka.

Mnamo mwezi Julai, wanajeshi wanne wa Umoja wa Mataifa walikuwa ni miongoni mwa watu 36 waliokufa katika maandamano yaliyozuka katika mkoa wa Goma na Butembo mashariki mwa DRC.

Waandamanaji hao waliishtumu MONUSCO kwa kushindwa kuzuia kuzuka upya kwa ghasia.

Mauaji ya raia yamekuwa jambo la kawaida huku idadi ya watu waliokimbia makazi yao ikipindukia kua mamilioni.

Guterres amesisitiza umuhimu wa pande zote zinazohasimiana kukaa kwenye meza ya mazungumzo ili kurejesha amani nchini humo.

Hata hivyo, hoja yake hiyo inaonekana kutokuwa na mshiko miongoni mwa wanaharakati nchini humo.

Serikali ya Tshisekedi imesema haiko tayari kufanya mazungumzo na M23 kundi ambalo limewekwa katika ngazi ya magaidi.

Hali hiyo inatishia kulemaza juhudi za kumaliza mzozo unaoendelea huko mashariki mwa Kongo.

Hata hivyo, katika kikao kilichoitishwa na Maron, Rais Tshisekedi na Kagame wamekubaliana kukutana tena katika kumaliza mzozo huo, huku kila mmoja akiahidi kudhibiti vikundi vya waasi.

Katika eneo la Mashariki mwa DRC, kuna utitiri wa vikundi vya waasi vinavyofanya harakati zao ndani ya misitu na hivyo kuwa tishio kwa usalama wa eneo zima la Afrika Mashariki. **DW**

MAKALA

# Salamu zangu wasichana mpango elimu haina mwisho

Na Mwandishi Wetu

WASICHANA waliopata changamoto wakiwa shuleni na kukwama kusoma, wameokolewa na Mpango wa Elimu Haina Mwisho unaoendeshwa takribani vyuo zaidi ya 50 ukiwasaidia waliokatisha masomo kutokana na ujauzito na sababu nyingine kama hali duni za kifamilia.

Ni karibu mwaka sasa baada ya kutangazwa kuwapo kwa fursa ya masomo ya elimu haina mwisho hivyo, kila mmoja aliyepatwa na changamoto anategemewa amejiunga na vyuo kusoma masomo ya sekondari na mafunzo ya ufundi.

Katika mpango huo kuna kujifunza elimu ya sekondari pia, ufundi kuanzia umeme majumbani, kushona , upishi, urembo, ujasiriamali na ushonaji vilevile, kwa wazazi, watoto wao wanahudumiwa vyuoni kwa kupata elimu ya makuzi na maendeleo ya awali kwa watoto.

Suala hilo ni hatua nzuri na inayokuja baada ya serikali kutangaza kuwa wanafunzi waliokatiza masomo kwa sababu yoyote ikiwamo mimba warejee masomoni, safari yao ikianzia kwenye vyuo vya maendeleo ya jamii kote nchini.



Jamii iunge mkono juhudi za kuwasaidia wasichana kusoma badala ya kuwakwamisha. **PICHA:MTANDAO**

Kutokana na uamuzi huo na maandalizi kwenye vyuo kukamilika ni dhahiri wasichana wako madarasani na wengine wanaendelea kujipanga. Kinachoendelea ni chema na wasichana hao ili kuendelea kuwapa 'shule bora' wasiachwe kuwafundisha masuala yanayohusu mimba za utotoni, ngono kabla ya ndoa na jinsi ya kukwepa vishawishi vinavyowaingiza kwenye kuzaa katika umri mdogo au kuingia tena kwenye mkwamo wa aina yoyote ile.

Kwa ujumla ni suala la kufundishwa maadili mema na wasichana wafahamishwe kuwa taratibu haziruhusu mwanafunzi kubeba ujauzito ni lazima kila jambo lifanywe kwa wakati.

Reuben Lumbagala, ni Mwalimu wa Sekondari ya Mlali mkoani Dodoma, anapozungumzia hatua hiyo anasifu kuwa ni nia njema na kuipongeza serikali akisema: "Nia njema ya serikali ya kutaka wanafunzi wa kike wanaopata ujauzito kuendelea na masomo, inapaswa kuangaliwa kwa umakini kabla ya utekelezaji wake ili kujenga msingi mzuri katika nia njema hiyo.".

Wanafunzi wa kike walioko shuleni wanapaswa kupewa elimu ya kijinsia na ya kimaadili kutoka kwa wazazi, walezi na walimu wao ili kuwa na misimamo thabiti isiyoyumbishwa, hatimaye kuepuka kuingia katika mahusiano wakiwa bado wanafunzi, hali inayosababisha kupata ujauzito.

"Ni vyema wanafunzi wa kike wakafahamu kuwa fursa iliyotolewa ya kuendelea na masomo si ya kuchezea bali ni kuwa majasiri na kupambana na vishawishi kutoka kwa wavulana na wanaume wanaowahadaa kimahusiano. Wasijisahau kwa kuwa ipo nafasi nyingine kwao ya kuendelea na masomo. Wajue kuwa kupata ujauzito katika umri mdogo ni hatari kwa mustakabali wa afya zao."

Aidha, anawakumbusha kuwa kujishughulisha na ngono kuna athari nyingi kisaikolojia, kiafya, kielimu na hatima ya maisha yao, hivyo wajihadhari na kutumia kikamilifu fursa ya kujisomea na kufanikisha ndoto zao.

Anawakumbusha wazazi na walezi kujenga misingi kwa mabinti zao kuepuka kupata ujauzito na kupata watoto wakiwa bado wanafunzi, kwani hata kijamii, suala hilo linashusha heshima kwa wazazi na walezi wao.

Katika ngazi ya familia, msisitizo wa maadili mema kwa watoto upewe msukumo mkubwa na liwe suala la kipaumbele. Lakini, si ujauzito pekee hata kujiingiza kwenye masuala ya uhalifu si jambo jema.

Mwalimu huyo wa masuala ya taaluma, anaongeza kuwa zaidi kuwa mambo yasiishie hapo Wizara ya Afya ishirikiane na wadau na iweke utaratibu wa mara kwa mara wa kufikisha elimu ya kijinsia shuleni ili kuwajengea uwezo wasichana katika mapambano ya mimba za utotoni.

Huko shuleni walimu walezi wa wanafunzi wa kike au matron (walezi) wapewe mafunzo ya mara kwa mara ili kuwaelimisha wanafunzi wao wa kike kuepuka mahusiano katika umri mdogo.

Ukweli ni kwamba, licha ya wanafunzi kulindwa kisheria kwa kutumia sheria ya makosa ya kujamiina, bado hali ni mbaya.

Licha ya sheria ya ushahidi kuwapo na kukataza washtakiwa wasipewe dhamana hasa washitakiwa wa ubakaji na ulawiti wa watoto ili kupunguza kuongezeka kwa vitendo hivyo huku watoto wakiathirika zaidi wakiwamo wanafunzi, hali ni mbaya kwani wanadaiwa wanapewa dhamana, hali ikijiri Zanzibar.

Kwa mfano, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, iliwahi kueleza kuwa matukio ya udhalilishaji wa kijinsia yaliyokusanywa na taasisi mbalimbali, likiwamo Jeshi la Polisi, kwa mwaka 2020 yalifikia 1,363, hiyo inaamaanisha kuwa wapo mabinti waliopata mimba na kukatishwa masomo.

Lakini, ni wakati wa mahakama kuharakisha hukumu kwa kesi za udhalilishaji ili zitolewe kwa wakati ili kuondoa mwanya wa kufanyika ufisadi na kulinda wanaowarubuni watoto na kuwapa mimba.

Yote hayo yafanyike kukomesha udhalilishaji na kuwapa watoto mimba.

Pia, kuna suala la muhali watu kuoneana haya hilo nalo lifanyiwe kazi ili wanaoshughulikia kesi za udhalilishaji wasiwe na muhali na kuoneana aibu katika usimamizi wa sheria ili kuondoa matendo hayo yanayorudisha nyuma wasichana.

Ni ukweli kuwa taarifa kutokana maeneo mbalimbali nchini, zimekuwa zikionyesha jinsi ambavyo baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakikumbwa na tatizo hilo.

Ndiyo maana tangu awali kulikuwa na mjadala kutoka wadau wa elimu, wakiwamo wanaotaka serikali iruhusu wanafunzi wanaopata ujauzito wakiwa shuleni waendelee na masomo baada ya kujifungua, huku wengine wakipinga.

Sasa kwa kuwa serikali imeamua kuja na utaratibu mpya wa kuwawezesha waliokatiza masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo ya mimba kuendelea na masomo, ni vyema wazazi, walezi na wanafunzi wasipoteze fursa hiyo lakini jamii iwe makini na mazoea ya kuwapa watoto mimba yakome.

Vilevile, wanafunzi ambao hawajakumbwa na tatizo hilo, isiwe fursa kwao kujiachia tu wakijua kwamba, wana nafasi ya kujiunga na vyuo vya maendeleo ya jamii kuendelea na masomo baada ya kujifungua.

Ni muhimu kila mwanafunzi kuchukua tahadhari zaidi ili kujiepusha na masuala ya ngono yanayoweza kuwaingiza kwenye mimba, maradhi ya kuambukiza kama VVU, utoaji mimba usio salama, ugumba na kuepusha kunyanyapaliwa.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Unakumbuka sinema za 'Chale Mwembamba'?

## •Mnene 'Chale Ndute', alifanywa bwege
## •Hazikuwa na rangi wala sauti

**Na Adam Fungamwango**

MIAKA hiyo siyo tu kwamba hakukuwa na televisheni, video, CD wala 'flashi', lakini asilimia kubwa hata nyumba zenyewe za miji mikubwa hazikuwa na umeme.

Kuanzia 1990 kurudi nyuma, watoto, vijana na hata watu wazima walilazimika kwenda kwenye majumba ya sinema kama vile New Chox, Empress, Cameo, Avalon, Empire, Starlight, Odeon na mengine yaliyokuwa yakionyesha.

Hiyo ni kwa jiji la Dar es Salaam, lakini mikoani nako kulikuwa na sehemu mbalimbali na kumbi maalum ambazo sinema zilipelekwa huko.

Na mara nyingi ni baada ya kuonyeshwa sana jijini Dar es Salaam na watu kuanza kuzikinai.


Sehemu ambayo kwa sasa umejengwa Ubalozi wa Marekani kulikuwa na ukumbi mmoja uliojengwa kimaajabu. Ulikuwa kama uwanja wa mpira. Ulizungushiwa ukuta mrefu, hakuweza yoyote kuupanda. Ndani waliingia watu wenye pesa zao ambao walikuwa na magari. Waliingia wao na magari yao. Uliitwa Drive Inn Cinema. Hata hivyo hata ukiwa nje uliweza kuona ukuta mkubwa uliokuwa juu ambao ndiyo ulitumika kuonyesha sinema.

Waliokuwa nje pia waliona, lakini kitu kilichowatenganisha ni ukuta tu wa ndani ndiyo walilipa na wao walikuwa wakisikia sauti, lakini nje haikuwa hivyo na waliangalia bure.

Nje walikaa vijana kutoka maeneo ya Tandale, Kinondoni, Mwananyamala, Kigogo, Mburahati, Manzese na kuangalia sinema ambayo hawakuwa wakisikia maneno. Lakini wenyewe wakitoka hapo wanatathiana utafikiri walisikia.

Hiyo ni kwenye kumbi kubwa za sinema. Huku mitaani sasa kulikuwa na kumbi ndogo ndogo zilizokuwa zikionyesha simena. Pia kulikuwa na magari yalikuwa yanakuja kwenye viwanja mbalimbali kwa ajili ya kuonyesha sinema.

Mengi yalikuwa aina ya Volkswagen Combi, ambayo yalikuwa ya makampuni mbalimbali yaliyokuwa na lengo la kutangaza bidhaa zao.



Kabla hawajaweka sinema yenyewe kama kina Bruce Lee na mastaa wengine wakati huo, walikuwa wakiweka ya ucheshi ambayo kwa sasa wanaita komedi.

Na komediani ambaye alikuwa maarufu wakati huo ni mtu mmoja anaitwa Charlie Chaplin.

Huyu jamaa ndiyo Mr Bean wa wakati huo, japo mpaka sasa kuna watu wanataka kuwalinganisha ili wapate nani zaidi yao.

Vijana na watoto wa wakati huo walimwita 'Chale Mwembamba' kutokana na umbile lake na alipenda kuigiza na mwingizaji msaidizi mmoja ambaye lazima awe mnene.

Mwigizaji mwenzake wa karibu yoyote yule aliyeigiza naye aliitwa 'Chale Mnene' au 'Chale Ndute.'

Charlie Chaplin alizaliwa London, 16 Aprili 1889, na mwaka 1910 Charlie alisafiri na kuelekea Marekani na kupata ujuzi katika sekta ya filamu kutokana na kipaji alichokuwa nacho cha uchekeshaji alibuni alama mtindo wake wa uvaaji uliokuwa ukimtambulisha ni kofia ya bakuli, masharubu na nguo anazozijua mwenyewe.

Chaplin, na vipaji vya ajabu kwani pamoja na filamu zake za kimya, yaani hazina sauti, lakini zilieleweka kirahisi na hadi watu wanaondoka kwenye sinema, wanakuwa 'wameshavunjika mbavu' kutokana na vituko vyake. Pia sinema zake zilikuwa hazina rangi.

Siyo kwamba ilifanyika hivyo na makusudi, bali wakati jamaa huyo anacheza picha zake hizo, bado teknolojia ya rangi kwenye video, pamoja na sauti kwenye simema ilikuwa bado sana.

Alianza kucheza sinema miaka ya 1940 hadi 1950, hivyo waliokuwa wakiangalia filamu zake miaka ya 1970 hadi 1990, ilikuwa tayari imepita miaka 40 hadi 50, wakati teknolojia ya filamu za rangi na sauti ndiyo ilikuwa imeshapatikana.

Ndiyo maana kabla ya kuwekwa filamu kamili, inawekwa kwa mchekeshaji huyo na hata ukizitazama tu utagundua kuwa zilichezwa miaka mingi sana iliyopita.

Wakati huo filamu za awali, ziliitwa 'pati gazeti', au 'trela'. Kwa kijana wa kizazi cha sasa kama hujawahi kuona filamu zake, basi unaweza kuzisaka na kuzitazama, uone jamaa alivyobarikiwa vituko. Yaani kila filamu inaishinda nyingine.

Alifariki Sikukuu ya Krismasi mwaka 1977 na kuacha simanzi na majonzi makubwa kwa mashabiki wake, filamu na vichekesho kwa ujumla.

Mada hii iliwekwa kwanza kwenye mtandao ya kijamii na wadau wakafunguka jinsi walivyokuwa wakitoka majumbani kwenda kuangalia filamu zake, pia wakimuelezea mchekeshaji huyo.

"Nimemcheki huyu jamaa, alikuwa anajua sana, enzi zile tulikuwa tukiingia sinema mahususi kwa ajili ya kumcheki huyu jamaa, sinema ikiisha unameza na dawa za kuondoa maumivu kwa jinsi mbavu zinavyouma kwa kucheka," alisema mdau mmoja. Mwingine akaandika jinsi anavyowafahamu majina yao

"Tuliwafahamu zaidi kwa majina ya 'Chale Ndute' na 'Chale Mbwambwambwa', mmoja alikuwa mwembamba na mwingine mnene."

"Ameacha historia duniani kwa kazi yake ya sanaa iliyowavutia watu wengi kipindi hicho mpaka sasa ni miongoni mwa watu waliokuwa na vipaji hasa mpaka kuna baadhi ya watu wanasema hajatokea kama yeye hadi leo," mchangiaji mwingine akabainisha.

"Nimeona jina tu nimecheka, sisi watoto wakati huo tuliwaita 'Chale Ndute na Chale Mwembamba.'"

Yupo mchangiaji mwingine ambaye alisema wakati yuko mdogo na kumuangalia, hakudhani kama ni binadamu wa kawaida.

"Yaani kuna wakati hadi nafikiria jamaa hakuwa binadamu wa kweli bali ni katuni tu, komedi zake ni nzuri sana kuna ile alipoingia kwenye banda la simba wenye njaa, duh huwa naifurahia sana."

Mwingine naye akakumbuka filamu yake nyingine.

"Kuna ile moja moja ambayo wapo kiwandani, yeye kapewa spana ya kukaza bolti, ilikuwa hatari, ni vituko vitupu."

Kuna dada mmoja yeye hakuwahi kuangalia filamu zake, lakini siku alipojaribu ikawa balaa

"Kuna siku natoka Dar kwenda Songea kwenye basi tuliwekewa vituko vyake jamani hadi tunafika Songea hakuna aliyelala ni kucheka tu, huyu baba ana kipaji aisee nahisi ni zaidi ya Mr Bean."

"Kuna ile yupo ulingoni anapigana masumbwi na mpinzani wake aise...hakuna atakaye mfikia hata siku moja." Huyu akamjibu mwenzake.

"Kuna ile ya makenika, yaani nilicheka hadi machozi, hatari sana sana huyu babu, huwa nacheka sana nikiangalia zake, nafikiri Mr Bean alikopi kwa huyu."

**Tuma meseji 0716 350534**



# Israel yataka kuundwa jeshi kutumika dhidi ya Iran

**NEW YORK,** MAREKANI

MKUTANO wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa umeingia siku yake ya nne jana na suala la vita nchini Ukraine likiwa limechukua nafasi kubwa.

Migogoro na matatizo mengine ambayo baadhi ni ya muda mrefu, yameanza kuzungumzwa kwenye mkutano huo baada ya Waziri Mkuu wa Israel, Yair Lapid, kusema anaunga mkono kuundwa kwa dola huru la Palestina ingawa akasisitiza kwamba jumuiya ya kimataifa inapaswa kutumia nguvu za kijeshi dhidi ya Iran kuizuia isitengeneze bomu la Nyuklia.

Rais wa mamlaka ya Wapalestina Mahmoud Abbas, anatarajiwa kuzungumza mbele ya baraza hilo pia.

Migogoro mingine ya kikanda iliyoongezeka ni kati ya Armenia na Azerbaijan na Waziri Mkuu wa Armenia, Nikol Pashinyan ameonya kwamba bado kuna kitisho kikubwa cha Azerbaijan kuanzisha tena mapigano mapya dhidi ya nchi yake.

Aidha viongozi wengine wanaotarajiwa kuzungumza kwenye mkutano huo ni kutoka Iraq na Pakistan nchi zote hizo ni muhimu katika siasa za kikanda za ulimwengu ingawa katika miaka ya hivi karibuni nchi hizo hazikupewa umuhimu mkubwa. **DW**

## Guinea yawekewa vikwazo

**CONAKRY,** GUINEA

JUMUIYA ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (Ecowas) imewawekea vikwazo watu binafsi katika serikali ya kijeshi ya Guinea katika kupinga mapinduzi ya mwaka jana.

Viongozi kutoka nchi wanachama wa umoja huo walikutana mjini New York walikokuwa wakihudhuria Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na kukubaliana kuwawekea vikwazo watu hao.

Vikwazo hivyo vitawahusisha orodha ya watu kutoka serikali ya Guinea ambao watatambuliwa hivi karibuni.

Kulingana na shirika la habari la AFP, viongozi wa Guinea wanasema wanahitaji miaka mitatu kuirejesha nchi hiyo katika demokrasia na hawajafurahishwa na matakwa ya Ecowas ya kutaka mabadiliko ya haraka katika kipindi cha mpito.

Katika taarifa yake, Waziri Mkuu wa mpito wa Guinea, Bernard Gomou, awali alimuelezea mkuu wa Ecowas na rais wa nchi jirani ya Guinea-Bissau, Umaro Sissoco Embalo, kama kibaraka na mtu aliyefurahi kupita kiasi ambaye alilazimisha kuingia kuongoza shirikisho hilo la kikanda.

Guinea ilisimamishwa kuwa mwanachama wa Ecowas kufuatia mapinduzi ya kijeshi ya Septemba mwaka jana. **BBC**



Mwanajeshi wa Russia akitazama meli zilizoweka nanga katika bandari moja ya Ukraine. **PICHA Getty Imeges**

# Marekani ipo makini vitisho kutoka Russia

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imesema inachukua kwa uzito vitisho vya Rais wa Russia, Vladimir Putin vya kutumia silaha za nyuklia kutetea maeneo ya Ukraine.

Ofisa wa ngazi ya juu wa Ikulu ya White House, John Kirby alisema Marekani haibadilishi mkao wake wa tahadhari wa kuzuia, na kumlaumu Putin kwa kuzungumza bila kuwajibika.

Siku ya Jumatano Putin aliionya nchi yake itatumia njia zote ili kulinda eneo lake.

Ilikuja wakati mikoa minne ya Ukraine ambayo sehemu yake inamilikiwa na vikosi vya Russia inakaribia kuandaa kura za haraka za kujiunga na nchi hiyo.

Ukraine na washirika wake waliziita kura hizo kuwa ni zoezi la udanganyifu, lililoundwa ili kutoa uhalali wa uongo wa unyakuzi haramu wa ardhi.

"Ni mfano hatari kwa Putin kutumia matamshi ya aina hii katika muktadha wa vita ambavyo ni dhahiri kwamba anashindwa ndani ya Ukraine," msemaji wa Baraza la Usalama la Kitaifa Kirby aliiambia BBC.

Mwenendo wa Russia nchini Ukraine umelaaniwa vikali katika mkutano maalum wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa mjini New York siku ya Alhamisi.

Katika hotuba yake ya wiki hii, Rais Putin alisema nchi yake haitasita kutumia mifumo yote ya silaha inayopatikana katika kukabiliana na tishio kwa uadilifu wa eneo lake.

Ujerumani kusaidia wanaokimbia

Inadaiwa kuwa Ujerumani iko tayari kuwasaidia Warussia wanaotoroka kuepuka kusajiliwa kama wanajeshi wa akiba, amesema Mwandishi wa BBC, Damien McGuinness kutoka Berlin.

"Warussia wanaokataa vita hivi vya ufashisti wanapaswa kupewa hifadhi katika Ulaya huru," alisema mmoja wa wanasiasa wakuu wa chama tawala cha Social Democratic cha Ujerumani.

Kwa wengi katika serikali ya Ujerumani, wanawaona watu hao ni Warussia wanaoondoka nchini mwao ili kuepuka kuitwa vitani nchini Ukraine.

Bado haijawa wazi jinsi gani itafanya kazi kama watapewa hifadhi au kupewa viza za kibinadamu.

Kansela wa Ujerumani, Olaf Scholz pia anapinga mapendekezo ya hivi karibuni ya baadhi ya nchi za Ulaya Mashariki kufunga mipaka kwa raia wa Russia.

Mara kwa mara aliita uvamizi huo ni vita vya Putin na kusema kwamba Warussia wanaopinga wanapaswa kuungwa mkono.

**ULAYA KUONGEZA VIKWAZO**

Wazungu wameanza kujadili vikwazo vipya dhidi ya Russia kujibu uamuzi wa Vladimir Putin wa kusajili wanajeshi wa akiba na vitisho vyake vya siri vya nyuklia dhidi ya Magharibi.

Wakati wa miezi sita ya vita, Ulaya ilikata uhusiano wake wa kibiashara na kifedha na Russia.

Majadiliano ya vikwazo yalianza Ijumaa na yanapaswa kukamilishwa na mkutano wa kilele wa viongozi wa mataifa 27 huko Prague.

Msingi wa vikwazo vipya unaweza kuwa upanuzi wa orodha ya watu binafsi na makampuni, pamoja na ukomo wa bei ya mafuta ya kutoka Russia.

Vikwazo hivyo vinaanza kutekelezwa kuanzia Desemba, lakini sio kwa usafirishaji wa kupitia mabomba.

Ulaya imepiga marufuku bima, ufadhili na usafirishaji wa mafuta kutoka Russia.

Marekani iliogopa kwamba vikwazo vya Ulaya vitasababisha kuongezeka kwa bei za dunia na kutoa njia mbadala ya kuweka ukomo wa bei kwa mafuta yanayotoka nchini humo.

Akijibu hatua hiyo, Putin alisema kwamba basi hatasafirisha chochote: si mafuta wala gesi, wala bidhaa zingine zozote.

Bado haijabainika nini kitatokea kutokana na vikwazo hivyo ikiwa EU itaamua kuweka ukomo kwa bei ya mafuta yaliyonunuliwa kutoka Russia kama sehemu ya vikwazo vipya.

Mara ya mwisho, Hungary ilipinga vikali na matokeo yake idhini ya vikwazo vya mafuta ilichelewa, huku vikwazo wenyewe vikigeuka kutekelezwa nusu na kuchelewa kwa miezi sita. **BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**JULIANA GASPAR BONIFACE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0491-0023 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KILOMENI SEKONDARI** mwaka 2012. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/OST/RB/378320/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ERNEST RICHARD** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0181/0068 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KISARAWE LUTHERAN JUNIOR SEMINARY** mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha **Polisi. Taarifa ya Polisi: DAR/URA/RB/377694/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA UBUNGO LILILOKO – LUGURUNI**

**MAOMBI MADOGO NAMBA 303 MWAKA 2022**

**VICTORIA FINANCE PLC..................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**RASHID ABDALLAH SEBARUA.......WAJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

**RASHID ABDALLAH SEBARUA..........POPOTE ULIPO**

VICTORIA FINANCE PLC Amewasilisha shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ubungo lililopo Kibamba – Luguruni. Maombi hayo yamepangwa kutajwa tarehe 17/10/2022. Hivyo basi unatakiwa wewe mwenyewe au wakili wako kuleta kiapo kinzani "counter affidavit" ndani ya siku 7 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa. Vilelezo vyote vinavyohusu shauri tajwa vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ubungo. Endapo hatutatekeleza haya, maombi hayo yatasikilizwa upande mmoja na uamuzi/amri kutolewa.
Imetolewa na kutiwa muhuri wa Baraza leo tarehe 22/09/ mwaka 2022.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) UBUNGO
DAR ES SALAAM

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Kesi ya Jinai No 283/2022**

**Kutoka Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Bukoba**

**Kituo cha Bukoba Mjini Mkoa wa Kagera**

**KUITWA SHAURINI-MLALAMIKAJI**

**Kwa SHAKIRU MOHAMED**

Kwa kuwa imelazimika uhudhurie shaurini, unaamuliwa na Mahakama uhudhurie siku ya tarehe 4 Mwezi 10 Mwaka 2022 saa 02;30 asubuhi ili shauri liweze kusikilizwa.Endapo utashindwa kuhudhuria siku na muda uliopangwa hapo juu,na ikithibitika kwamba umepokea kuitwa shaurini hati ya kukamatwa itatolewa dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Mhuri wa Mhakama hii tarehe 22/09/2022

**HAKIMU**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**AT SUMBAWANGA**

**CIVIL /APPEAL CASE NO. 6 OF 2020**

**FABIAN PETER KASHINJE APPELLANT**

**VERSUS**

**EDA MANFRED NDOMBA RESPONDENT**

**TO EDA MANFRED NDOMBA**

**TAKE NOTICE** that the hearing of the above suit has been set down for mention /hearing on the 15th day SEPTEMBER 2022 in the forenoon of thereafter.
You must produce on that day all the witnesses upon whose evidence and all the document upon which you intend delay in support of year case.
Given under my hand and the seal of this Court this 18 day 2022

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
SUMBAWANGA

PLACE HIGH COURT –SUMBAWANGA
COPY TO RESPONDENT
RESPONDENT
RECEIVED COPY TO THIS NOTICE

**Uza,**
**Chenye Thamani**
**Kubwa Kwa**
**Kutangaza Nasi Kwa**
**Bei Poa**
**Tupigie, 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa. Matokeo ya haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# KAMA IPO, IPO TU-24

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

"Kwanza kabisa naomba samahani kwa haya yaliyotokea. Ni kwamba itafika mpaka mwisho wa dunia hamtoweza kumuona mchumba ambaye anatajwa kuwa angekuja kumuoa Siwatu. Huyu mchumba ni mimi. Na hata barua ambayo Siwatu ulikuwa unaisoma ukidhani kuwa imeandikwa na huyo mtu, iliandiwa na mimi mwenyewe. Hata ukiunganisha mkasa uliousoma utagundua kuwa unafanana na ule niliokusimulia baada ya kukupora barua na kuanza kusimulia mimi mwenyewe. Kifupi mkasa ni huo ni mmoja. Ila kwenye barua ulikuwa umeandikwa na baadaye mimi nilianza kusimulia pale ulipoishia kwenye barua, ndiyo maana unaona ulifanana sana. Kisa ulichokisoma kwenye barua tangu mwanzo ni changu mimi na ndicho kilichosababisha mpaka nitupwe hapa kijijini kwenu na wewe kuniokoa." Akasema Bakari na kusababisha mshangao kwa Dibwela na Siwatu.

Kifupi ni kwamba Billy na Daudi walijua kila kitu. Na kila walichokifanya kilitokana na maelekezo ya Bakari.

"Nilifanya yote haya kwa sababu zangu ambazo nitazisema mbele ya safari. Kwa kifupi tu mimi jina langu kamili naitwa Samson Dau na si Bakari. Jina la Bakari nililitunga mwenyewe ili litumike hapa kijiji wakati ule nilipookolewa na Siwatu. Sikutaka kujitaja kwa jina langu halisi kwa sababu zangu binfasi."

Mpaka hapa, tayari Siwatu akili yake ilishaanza kukaa sawa, na kutambua yule mtu aliyeishi naye baada ya kumuokoa aliyemtambua kwa jina la Bakari, ndiye Samson Dau au Bosi Mulango kama Billy na Daudi walivyopenda kumwita.

"Kama nilivyoandika kwenye barua iliyosomwa na Siwatu mimi nimetoka kwenye familia ya kitajiri, na hawa mnaowaona hapa ni baadhi ya mamia ya wafanyakazi wangu. Pia makazi yangu siyo Chalinze kama nilivyosema wakati ule ila ni Dar es Salaam. Yote nilifanya kwa mkakati maalum wa kujilinda mimi mwenyewe na kuna vitu nilikuwa nahitaji kufanya uchunguzi kabla ya kuvithibitisha."




**"Kobelo huyo." Akadakia Dibwela.**

Wote walibaki kumuangalia Bakari ambaye kwa sasa amejitambulisha kwa jina la Samson Dau, kuwa ndiyo jina lake halisi.

"Yalikuwa ni mambo ya husuda za kibiashara nikatekwa na V8 yangu wakaichukua, nikatupwa kwenye pori la kijiji hiki. Lengo walikuwa waniue. Lakini yule mkubwa wao kumbe alinitambua. Mimi sikumtambua. Akawakataza wasiniue kwa risasi badala yake wanipige na kuniacha porini ili niliwe na wanyama. Kumbe nia yake ni kuniokoa wasiniue tu. Akawaruhusu wanipige, alipoona inatosha akawakataza na kuwambia watangulie kwenye gari ili yeye animalizie na kuhakikisha kama sitobaki hai. Ni kweli nilihisi kitu ingawa nilikuwa kwenye hali mbaya, yule jamaa aliponiinamia, nikajua ananimaliza. Hakufanya hivyo. Alivyoona niko hoi tu akaniacha na yeye akaondoka. Kumbe ni mmoja kati ya watu niliowahi kuwasaidia na alikuwa analipa fadhila. Nililijua hilo baadaye na ndiye aliyenielekeza sehemu ya kwenda kuchukua gari yangu."

Siwatu na kaka yake Dibwela ndiyo walioonekana kuyashangaa zaidi maelezo hayo. Kumbe walichokifanya ni kitu kizuri kwenye maisha yao, ingawa bado kama walionekana kuwa na mashaka hivi. Bado walimuacha Bakari aendelee kutiririka.

"Baada ya wasichana watatu kunigundua pale nilikuwa hoi, sikuwa na la kufanya, wala kuwapa ishara, waliondoka, baada ya muda nyota ya jaha ilikuja. Alirejea msichana huyu." Aliposema hivyo kwa sababu alikuwa amesimama kando ya Siwatu aliyekuwa amekaa chini, alimshika mkono. Siwatu akasimama, akamkumbatia. Akambusu.

"Alikuja na ndoo, akanimwagia maji kwa nia ya kuniogesha na kunizindua, na kweli nilizinduka, akaninywesha maji. Ilikuwa jioni saa 12:00, kwa mtoto wa kike porini na kitu kama kile kuwa na biandamu ambaye ni nusu mfu ilikuwa ni kitu cha kutisha kweli kweli. Hakutishika. Pamoja kwamba alijua siwezi kuamka na nakaribia kifo, akaniambia kwa sauti kuwa anakwenda kijijini kuita watu. Saa moja baadaye ilikuwa tayari giza limeingia hivi alirudi yeye mwenyewe akiwa ameambatana na huyu kaka yake Dibwela na kijana mwingine."

"Kobelo huyo." Akadakia Dibwela.

"Ewaa bwana shemeji. Ndiyo nikaletwa kijijini. Sikutaka kujitambulisha jinsi nilivyo, nikajitambulisha kama Bakari. Nikaishi hapa kama raia wa kawaida tu. Raha na karaha za kijiji zikanipata. Baadhi ya wanakijiji pamoja na uongozi ulionekana kupinga sana mimi kukaa hapa. Ikasababisha hata kutengwa. Maneno yakawa mengi na ya kukatisha tamaa kwangu na Siwatu. Mtoto wa watu hakukata tamaa. Aliendelea kuwa mwanamke shujaa. Shupavu. Hata kama wote wakamkataa alisimama na mimi. Na mpaka wakati huo tayari watu wote walidhani mimi na Siwatu ni wapenzi kwa sababu tulilala chini pamoja. Ni kweli tumependa, lakini hakuna hata mmoja aliyewahi kumtamkia mwenzake hilo. Lakini kila kitu kilichobakia kilionyesha kuwa tunapendana. Tunavyotazamana. Tunavyotembea kwenda sehemu mbalimbali. Tunavyoongea, tulionyesha tunapendana na kila mmoja alimhitaji wenzake, lakini hakuna aliyemwambia mwenzake. Hata hivyo ilibidi lazima nirejee nyumbani nikamuone mama yangu na dada zangu, nikaone biashara zangu tangu nilivyoziacha. Wakati huo nilipoteza mawasiliano wa ndugu, jamaa na marafiki kwa miezi yote hiyo wakadhani nimefariki. Habari ikaenea kuwa nimeuawa na kutupwa porini, lakini hakuna aliyejua ni wapi. Hilo nililifahamu niliporejea nyumbani. Huku nilimuaga Siwatu. Tuliagana porini siku aliponisindikiza. Tulilia machozi. ilikuwa karibu na kule alikoniokota. Nilimuahidi nitarejea baada ya mwezi mmoja." Akaendelea kuongea kwa hisia, kiasi cha machozi kumlengalenga.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# KAMATI YA WAAMUZI LIGI KUU BARA YAOMBA RADHI

**Na Adam Fungamwango**

HUKU Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa imesimama kupisha kalenda ya kimataifa ya FIFA, Kamati ya Waamuzi wa Soka nchini imeomba radhi kwa wadau wote kutokana na makosa yanayofanywa na waamuzi wake ambayo yamepelekea baadhi yao kufungiwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi Tanzania, Nassor Hamdoun, amesema inasikitisha kuona pamoja na kuendesha mafunzo na semina mbalimbali ya namna ya kutafsiri sheria za soka, lakini bado baadhi ya waamuzi wamekuwa wakishindwa kufanya vyema katika mechi za ligi na kusababisha malalamiko kutoka kwa mashabiki wa wadau wa soka.

"Niombe radhi kwa wadau wote wa soka kwa hili ambalo limetokea, kusema kweli sisi tunajitahidi sana kuwapa mafunzo na semina ili wazitafsiri sheria na kanuni za mpira, sasa ikitokea hawafanyi hivyo kwa sababu ambazo wanazijua wenyewe inasikitisha sana," alisema Hamdoun, ambaye ni mwamuzi wa zamani wa kimataifa.

Mwenyekiti huyo alisema hadhani kama tatizo ni kutojua sheria kwani kuna waamuzi ambao wameshapata hata zawadi za uamuzi bora msimu uliopita, iweje sasa waonekane hawawezi.

"Angalia mwamuzi kama Ahmed Aragija, msimu uliopita alikuwa mwamuzi bora, leo inakuwa hivi, hii kweli unaweza kusema hajui? Tunawapa mafunzo hawa sana, lakini pia si kweli kwamba labda hawalipwi, waamuzi wanalipwa, labda kinachotokea ni ucheleweshaji kidogo na hii inatokana na masuala tu ya taratibu za kifedha, lakini hakuna mwamuzi ambaye anafikisha raundi tatu au mbili hajalipwa," Hamdoun alisema.

Juzi, Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania katika kikao chake kilichofanyika Septemba 21, mwaka huu pamoja na mambo mengine, iliwapeleka kwenye Kamati ya Waamuzi, marefa Aragija, Amina Kyando na wasaidizi Frank Komba na Black Tubuke kwa kushindwa kumudu vyema michezo waliochezesha.

Aragija anapelekwa huko kwa kushindwa kumudu mechi za Yanga dhidi ya Azam na Prisons dhidi ya Simba, huku Komba yeye akipelekwa kwa kushindwa kumudu mechi ya Yanga dhidi ya Azam FC.

Tubuke, anapelekwa huko kwa kushindwa kumsaidia vyema mwamuzi namba moja kwenye mechi ya Prisons dhidi ya Simba, na Kyando kwa kushindwa kumudu vizuri pambano kati ya Namungo dhidi ya Coastal Union.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), wakifanya mazoezi kujiandaa na fainali za Kombe la Dunia (U-17), zitakazofanyika India kuanzia Oktoba 11 hadi 30, mwaka huu. **PICHA: TFF**

# *Ruvu Shooting yaitisha Yanga*

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kupata pointi tatu muhimu katika mechi yake iliyopita ya Ligi Kuu Bara waliyocheza dhidi ya Polisi Tanzania, Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Charles Mkwasa, amesema timu yake imejipanga vyema kuhakikisha wanawaduwaza mabingwa watetezi, Yanga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkwasa alisema kikosi chake kimeendelea kujiimarisha na hawana hofu yoyote kuelekea mchezo huo unaofuata ambao utachezwa Oktoba 3, mwaka huu.

"Mchezo wetu na Yanga utakuwa mgumu na wenye ushindani kwa sababu tunakutana na bingwa mtetezi na mshiriki wa mashindano ya kimataifa, hatutabweteka, wajipange," alisema Mkwasa.

Kocha huyo alisema baada ya mchezo wao dhidi ya Polisi Tanzania uliochezwa mjini Moshi, Kilimanjaro ameendelea kuyafanyia kazi mapungufu aliyoyabaini na hatimaye kukaa tayari kushubiri mechi hiyo.

"Tunashukuru wachezaji waliokuwa wagonjwa wameungana na wenzao na hali zao kwa sasa zinaendelea kuimarika, kila mchezaji ana hamu na mchezo huo," Mkwasa alisema.

Aliongeza anawaomba mashabiki wao waendelee kuwaunga mkono kwa kujitokeza kuwashangilia kwa sababu msimu huu wameimarika na wamejipanga kufikia malengo.

## Klabu 12 kuwania ubingwa kuogelea

**Na Shufaa Lyimo**

KLABU 12 zinatarajia kuchuana kuwania ubingwa wa Taifa wa kuogelea katika mashindano ya wazi yatakayofanyika leo na kesho kwenye bwawa la kuogelea la Shule ya Kimataifa ya Tanganyika (IST) lililoko Masaki, Dar es Salaam.

Klabu hizo zinazotarajiwa kuchuana ni Taliss-IST, Bluefins, MIS Piranhas, Mwanza, Dar es Salaam Swimming Club, FK Blue Marlins, Champion Rise, Braeburn Arusha, Pigec, Lake na klabu mbili kutoka Uganda ambazo ni Flash na Starling.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Chama Cha Kuogolea Tanzania (TSA), Hadija Shebe, alisema wanatarajia waogeleaji zaidi ya 200 watashiriki katika mashindano hayo yaliyodhaminiwa na Pepsi, Knight Support, IST, Rap &Roll na Restaurant ya Delhi Darbaar.

Shebe alisema mashindano hayo yatashirikisha waogeleaji wa umri kuanzia miaka tisa na wenye zaidi ya miaka 15 ambapo watapangwa katika makundi manne.

"Waogeleaji watakaomaliza katika nafasi ya nne watapata pointi 12 ambapo wa tano, sita, saba, nane, tisa na 10 watazwadiwa pointi 10, 8, 6, 4, 2 na moja. Haya ni mashindano ya TSA na yapo kwenye kalenda ya chama, hivyo waogeleaji wenye vigezo wanatakiwa kushiriki katika mashindano hayo," alisema Shebe.

## Umoja Mbuzini FC yaongoza Unguja

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Umoja wa Mbuzini FC imeendelea kufanya vizuri katika Ligi ya Kanda ya Unguja baada ya kuichapa Gulioni mabao 5-1 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan juzi.

Kwa matokeo hayo, Umoja wa Mbuzini imefikisha pointi saba na kukaa kileleni kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa Umoja wa Mbuzini, Ramadhani Khamis, alisema mafanikio ya timu yake tangu kuanza kwa msimu huu yametokana na hamasa kubwa waliokuwa nayo wachezaji pamoja na mashabiki.

Khamis alisema msimu uliopita walifanya vizuri lakini wapinzani wao waliwazidi na sasa wanajipanga kuhakikisha wanapanda daraja na kucheza Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao.

"Bado ni mapema kusema lakini kutokana na mwenendo wa timu yetu na matamanio ya wachezaji ni kuhakikisha msimu ujao tunacheza Ligi Kuu Zanzibar, tumeanza vizuri kwa kutofungwa hata mchezo mmoja lakini bado tunahitaji kupambana zaidi ili kuhakikisha tunafanikisha lengo letu msimu huu," alisema Khamisi.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MESSI AITAJIRISHA PSG

USAJILI wa Paris St-Germain wa nyota wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 35 kutoka Barcelona kwa uhamisho wa bila malipo uliofanyika Agosti mwaka jana sasa umeiingizia klabu hiyo ya Ligue 1 mapato ya euro milioni 700 kutokana na mikataba ya kibiashara. ***(El Economista via Mirror)***

### RODGERS APEWA MUDA

LEICESTER City wananuia kumpa kocha aliyekalia kuti kavu, Brendan Rodgers muda zaidi wa kubadilisha mambo katika klabu hiyo iliyo mkiani mwa Ligi Kuu England. (***The Athletic***)

### GORDON, EVERTON SAFI

MAZUNGUMZO ya mkataba mpya kati ya Everton na Anthony Gordon "yanaendelea vyema" huku mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 21, aliyehusishwa na uhamisho wa kutakiwa Chelsea msimu wa joto, akitazamia nyongeza "kubwa" ya malipo. (***inews***)

### PARKER ANUKIA NICE

KOCHA wa zamani wa Bournemouth na kiungo wa kati wa England, Scott Parker mwenye umri wa miaka 41 ameibuka kuwa mtu anayetarajiwa kuchukua mikoba ya ukocha katika klabu ya Nice. (***Foot Mercato via Sun***)

### SCHMEICHEL MAMBO MAGUMU

GOLIKIPA wa Denmark, Kasper Schmeichel mwenye umri wa miaka 35, amekuwa na matokeo mabaya kwa mara ya kwanza katika klabu ya Nice tangu uhamisho wake kutoka Leicester City, baada ya kuwasili akiwa mzito na kuwasumbua wasimamizi na wachezaji wenzake kwa kukiuka sheria za klabu. (***RMC Sport via Sun***)

### MKATABA WAMBANA MIN-JAE

MLINZI wa Korea Kusini, Kim Min-jae ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United, ana kipengele cha kutolewa katika mkataba wake wa Napoli wa takriban euro milioni 50. Lakini, kwa vile haiwezi kuanzishwa katika dirisha la uhamisho la Januari, klabu yoyote inayotaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 italazimika kusubiri hadi msimu ujao wa joto. (***Gianluca Di Marzio)***

### PIQUE NJIA PANDA

BARCELONA watakuwa na chaguo la kusitisha mkataba wa beki wa kati wa Hispania, Gerard Pique ifikapo Juni mwakani, mwaka mmoja mapema - iwapo beki huyo mwenye umri wa miaka 35 atashiriki kwa chini ya asilimia 35 ya mechi zote msimu huu. (***Mundo Deportivo***)

### DYBALA MAMBO WAZI

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 28, amesema "miaka michache iliyopita katika Juventus haikuwa rahisi" na mabadiliko ya kuhamia AS Roma msimu wa joto "yalinisaidia". (***ESPN Argentina, via Football Italia)***

### WIJNALDUM ALIKARIBIA BARCA

KOCHA wa zamani wa Barcelona, Ronald Koeman amesema alitaka kumsajili kiungo wa kati wa Uholanzi, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 31, alipokuwa akiinoa klabu hiyo ya Hispania, lakini alishindwa kwa sababu Rais, Joan Laporta "alitaka kuniudhi zaidi kuliko kuleta mchezaji". (***AD, via Goal***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GIROUD AWEKA REKODI NA KUIBEBA UFARANSA

**●●● Ni baada ya kufunga bao katika kikosi hicho akiwa na umri mkubwa na...**

**PARIS,** Ufaransa

OLIVIER Giroud amekuwa mfungaji mwenye umri mkubwa zaidi katika historia ya Ufaransa wakati walipoichapa Austria na kuongeza matumaini ya kuepuka kushuka daraja katika mechi ya Ligi ya Mataifa ya Uefa iliyochezwa juzi.

Les Bleus hao walitawala mchezo, huku Kylian Mbappe akifunga bao la mapema lakini lilikataliwa kwa sababu ya kuotea na mpira wa tiktak ya Aurelien Tchouameni uligonga mwamba wa juu wa goli.

Halafu Giroud akamtengenezea pande zuri Mbappe ambaye alifunga bao la ufunguzi, akichuana na mabeki kadhaa kabla ya kupiga shuti akiwa umbali wa yadi 16.

Mshambuliaji huyo wa AC Milan, Giroud mwenye umri wa miaka 35, aliifungia Ufaransa bao hilo kwa kichwa.

Akiwa na umri wa miaka 35 na siku 357, amekuwa mfungaji mwenye umri mkubwa zaidi kuifungia Ufaransa, akimzidi siku 70, Roger Marche alipofunga katika mechi dhidi ya Hispania iliyochezwa Desemba, mwaka 1959.

Giroud sasa amefikisha mabao 49 na amebakiwa na mabao mawili pekee kuifikia rekodi ya mfungaji bora wa wakati wote wa Ufaransa, Thierry Henry mwenye mabao 51.

Ufaransa, ambao wangeshushwa daraja kama wangepoteza, walipanda juu ya Austria na kutinga fainali ya Kundi A1 na watacheza tena kesho dhidi ya Denmark.

Croatia wanaongoza kundi baada ya ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Denmark, ambao wangejikita kileleni wenyewe kama wangeshinda kule Zagreb.

Beki Borna Sosa aliwaweka wenyeji mbele kwa bao lake la kwanza la kimataifa.

Kiungo wa kati wa Manchester United, Christian Eriksen alisawazisha kwa shuti kali la mbali, lakini dakika mbili baadaye Lovro Majer alifunga bao la ushindi akiwa nje ya eneo la hatari.

Croatia inahitaji tu kuifunga Austria Jumapili ili kufuzu kwa fainali za mwaka ujao na kukata tiketi ya kufuzu kwa Euro 2024.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,033,2

MECHI KALI
SPAIN
VERSUS
SWITZERLAND
1 | 1.48
X | 4.14
2 | 6.46

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CONTE AFIKIRIWA KUMRITHI ALLEGRI



**TURIN, ITALIA**

KLABU ya Juventus itamfanya Kocha Mkuu wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte kuwa mlengwa wao mkuu iwapo wataamua kuachana na Massimiliano Allegri katika siku za usoni, kwa mujibu wa 90min.

Bianconeri wameanza msimu mpya pole pole, wakishinda mechi mbili pekee kati ya saba za kwanza za Serie A na kupoteza michezo yote miwili ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mtindo wa kiutendaji wa Allegri pia umewekwa shakani na yuko chini ya shinikizo kubwa la kupoteza kibarua chake hapo Juventus.

90min inaelewa baadhi ya wakuu wa Juventus wangependa kumbadilisha Allegri na nafasi yake ichukuliwe na Conte, licha ya kocha huyo kuzua mzozo alipokuwa akiondoka katika klabu hiyo mwaka 2014.

Conte alitaka kumsajili Juan Cuadrado - ambaye sasa anaichezea Juventus akitokea Fiorentina, lakini ombi lake lilikataliwa, na alikasirishwa na uuzwaji wa Arturo Vidal, akajiuzulu mara baada ya uamuzi huo kufanywa. Nafasi yake ilichukuliwa na Allegri kwa mara yake ya kwanza klabuni hapo.

Licha ya kuondoka kwake na malalamiko ya hali ya juu ya kurejea kwake kwa wapinzani wao Inter Milan katika miaka ya hivi karibuni, Conte yuko kwenye mahusiano mazuri na baadhi ya viongozi wa Juventus. Mkewe na binti yake pia bado wanaishi Turin.

Hata hivyo, matatizo ya kifedha ya Juventus yanamaanisha kumtafuta Conte itakuwa vigumu.

# Rashford, Dalot kupewa mikataba mipya

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United wana matumaini ya kuwapa wachezaji wake wa kikosi cha kwanza, Diogo Dalot na Marcus Rashford mikataba mipya ya muda mrefu, kwa mujibu wa 90min.

Dalot na Rashford ni miongoni mwa wachezaji tisa wa United ambao mikataba yao itakamilika msimu wa joto wa 2023, ingawa klabu hiyo ina chaguo la kuongeza muda wa mwaka mmoja kwenye mikataba hiyo.

Cristiano Ronaldo, Fred, David de Gea na Luke Shaw ni miongoni mwa majina mengine ambayo yamesalia chini ya mwaka mmoja kumalizia mikataba yao hapo United, ingawa ni Dalot na Rashford haswa ambao wameonyesha kiwango kizuri katika



mechi sita za kwanza za msimu mpya wa Ligi Kuu England.

Rashford ana mabao matatu - akifunga kwenye mechi dhidi ya Liverpool na Arsenal, na ana asisti mbili kwa jina lake.

Kiwango cha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 kimeongezeka chini ya Kocha, Erik ten Hag na msaidizi wake, Steve McClaren baada ya kujiandaa na msimu mzima.

Rashford alikuwa amepoteza nafasi yake katika timu baada ya kipindi kibaya cha kiwango msimu uliopita chini ya makocha, Ole Gunnar Solskjaer na Ralf Rangnick, huku mchezaji huyo akiuguza majeraha kwa muda mrefu katika misimu michache iliyopita.

## HABARI MICHEZO

283,276/-

# KIDUKU, MWARABU ULINGONI, MANDONGA GUMZO MTWARA

**Na Saada Akida, MTWARA**

ZIMEBAKIA saa chache kabla Mtanzania, Twaha Kassim 'Twaha Kiduku' kuvaana na Abdo Khaled kutoka Misri katika pambano la raundi 10 la kuwania mkanda wa dunia wa UBO litakalofanyika leo kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani hapa.

Licha ya kuwapo kwa mapambano ya utangulizi mbalimbali, Karim Mandonga anaonekana kubeba taswira ya siku ya leo kutokana na umaarufu alionao kwa sasa.

Mandoga amekuwa na umaarufu mkubwa ndani ya nchi kutokana na mbwembwe zake lakini akiwa hajawahi kushinda katika mapambano yanayoandaliwa na Peaktime Promotion.

Katika kupima uzito huo Mandonga aliyepewa ubalozi wa Mkoa wa Mtwara, ameendelea kuonyesha umaarufu wake kuliko wanasumbwi wengine waliombatana.

Mandoga, atapambana na Salim Abeid katika pambano la raundi nne wakati Adam Lazaro atatwangana na Francis Miyeyusho huku Emiliano Polino akipigana na Osama Arabi na Selemani Galile atapambana na Shaban Ndaro.

Pia, kutakuwa na pambano la raundi sita uzito wa kati litakalomkutanisha Nasra Msami dhidi ya Halima Bandola, likiwa ndiyo pambano pekee la wanawake katika siku ya leo iliyobeba jina la Ubabe Ubabe 2.

Bondia Alto Kyenga atapambana na Ibrahim Tamba, Malik Deo atacheza dhidi ya Bosco Bakari katika pambano la raundi nne huku Paschal Manyota akizichapa na Joseph Mchapeni, Shafii Mohamed vs Ramadhan Sunya, Iddi Pazi vs Sebastian Temba, Ayoub Mwankina vs Shabani Rajabu, Yassin Mbegu vs Hassan Mgaya na Azizi Salumu atapambana na Biemo



Msanii wa nyimbo za injili nchini, Angel Magoti, akiimba wakati wa ibada ya kumuaga marehemu, Balozi Paul Rupia, kwenye viwanja vya Karimjee jijini, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Stars majaribuni, U-23 yabanwa

INATOKA UK. 32

huo ulioonekana kuwa na ushindani wakati wote.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Hemed Morocco, alisema anawapongeza wachezaji wake kwa kuonyesha kiwango kizuri katika mechi hiyo.

"Kwanza ninamshukuru Mungu tumemaliza mechi salama, tumetengeneza nafasi lakini hatukuzitumia vizuri, tunaenda kujipanga kwa ajili ya mechi ya marudiano, sasa tumeshawafahamu wapinzani wetu, tutakuwa na wakati mzuri katika mchezo wa marudiano," Morocco alisema.

Sudan Kusini itaikaribisha Tanzania katika mchezo wa marudiano utakaochezwa wiki ijayo nchini Rwanda.

## NABI AWAANDALIA SUPRISE

INATOKA UK. 32

"Tutalazimika kushinda mechi yetu ya ligi (Ruvu Shooting), matokeo mazuri ya mechi hiyo yataongeza ari kwa wachezaji kuelekea mchezo dhidi ya Al Hilal, ni muhimu kuendelea kujiimarisha kwa sababu tunahitaji kutetea ubingwa," alisema Nabi.

Vinara hao wa Ligi Kuu Bara walisonga mbele katika michuano hiyo ya kimataifa baada ya kuichapa Zalan mabao 9-0, ikishinda magoli 4-0 katika mechi ya kwanza ya ugenini na kutoa dozi nyingine ya magoli 5-0 waliporudiana, mechi zote zikichezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Al Hilal itaikaribisha Yanga katika mechi ya marudiano itakayochezwa Oktoba 14, mwaka huu jijini Khartoum.

Wakati huo huo, Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, ametamba kikosi chao kimedhamiria kuendeleza makali yake katika mashindano ya kimataifa kwa sababu kinayafahamu vyema.

Ahmed alisema kila ndoto ya mchezaji wa Simba ni kuona wanafika hatua ya nusu fainali na kwa sababu hiyo wamejiandaa kupambana.

"Tunasema hatupoi, hatutaki kuona tunaishia njiani, msimu huu ni wetu, tumedhamiria kufika mbali, tunaamini hakuna kisichowezekana," Ahmed alisema.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 24/09/22 | 17:00 | Morecambe vs Cambridge Utd | 2.85 | 3.30 | 2.44 |
| 02. 24/09/22 | 17:00 | Barnsley vs Charlton | 2.33 | 3.28 | 3.03 |
| 03. 24/09/22 | 17:00 | Bristol Rovers vs Accrington | 2.50 | 3.40 | 2.70 |
| 04. 24/09/22 | 17:00 | Barrow vs Leyton Orient | 2.73 | 3.13 | 2.63 |
| 05. 24/09/22 | 17:00 | Hartlepool vs Gillingham | 2.64 | 3.19 | 2.69 |
| 06. 24/09/22 | 17:00 | Sutton United vs Salford City | 2.42 | 3.28 | 2.88 |
| 07. 24/09/22 | 17:15 | Mirandes vs Zaragoza | 2.98 | 3.18 | 2.41 |
| 08. 24/09/22 | 19:00 | Sarmiento vs Arsenal Sarandi | 2.36 | 3.14 | 3.24 |
| 09. 24/09/22 | 19:30 | Malaga vs Villarreal B | 2.31 | 3.24 | 3.09 |
| 10. 24/09/22 | 19:30 | Ponferradina vs Tenerife | 2.73 | 3.13 | 2.63 |
| 11. 24/09/22 | 21:30 | Lanus vs San Lorenzo | 2.49 | 3.14 | 3.04 |
| 12. 24/09/22 | 21:45 | Israel vs Albania | 2.41 | 3.18 | 3.08 |
| 13. 24/09/22 | 22:00 | Danubio FC vs River Plate (URU) | 2.36 | 3.12 | 3.07 |
| 14. 25/09/22 | 04:00 | Mexico vs Peru | 2.29 | 3.21 | 3.21 |
| 15. 25/09/226 | 05:00 | San Jose Earthquake vs Los Angeles Galaxy | 2.77 | 3.88 | 2.30 |
| 16. 25/09/22 | 15:00 | Burgos vs Levante | 3.39 | 3.04 | 2.26 |
| 17. 25/09/22 | 17:15 | Lugo vs Real Oviedo | 3.24 | 2.99 | 2.37 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 24/09/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 5695 | Forest Green vs Exeter | 3.10 | 3.25 | 2.22 |
| 15:00 | 4460 | Hong Kong vs Myanmar | 1.60 | 3.87 | 5.70 |
| 16:00 | 1007 | Amsterdam FC vs Jong Sparta Rotterdam | 1.90 | 3.65 | 3.60 |
| 16:00 | 1219 | Inverness vs Brechin City | 1.28 | 5.30 | 7.85 |
| 16:00 | 1682 | Montrose vs Kilmarnock FC B | 1.82 | 3.64 | 3.64 |
| 16:00 | 2650 | OFC Oostzaan vs Kozakken Boys | 3.44 | 3.59 | 1.89 |
| 16:00 | 3401 | Armenia vs Ukraine | 6.44 | 4.03 | 1.50 |
| 16:00 | 4796 | Quick Boys vs FC Lisse | 1.96 | 3.83 | 3.04 |
| 16:30 | 1357 | Gap Connahs Quay vs Pontypridd Town | 1.53 | 3.81 | 5.48 |
| 16:30 | 2735 | Bala Town vs Cardiff Met Uni. | 2.02 | 3.48 | 3.14 |
| 16:30 | 3393 | TEC vs HHC Hardenberg | 3.23 | 3.53 | 1.97 |
| 16:30 | 5270 | Haverfordwest vs Flint Town United | 2.06 | 3.43 | 3.09 |
| 17:00 | 1022 | Indjija vs FK Novi Sad | 1.32 | 4.52 | 8.44 |
| 17:00 | 1063 | Eastleigh vs Halifax | 2.14 | 3.34 | 3.14 |
| 17:00 | 2063 | Juventus Zurich vs Stade Nyonnais | 5.09 | 4.41 | 1.48 |
| 17:00 | 2145 | Bradford City vs AFC Wimbledon | 1.82 | 3.55 | 4.00 |
| 17:00 | 2342 | Clyde vs Caernarfon Town | 2.27 | 3.63 | 2.60 |
| 17:00 | 2782 | Crewe vs Mansfield | 3.04 | 3.34 | 2.21 |
| 17:00 | 2810 | Stevenage vs Harrogate | 1.61 | 3.75 | 5.20 |
| 17:00 | 3012 | Cove Rangers vs Raith Rovers | 2.14 | 3.89 | 2.66 |
| 17:00 | 3066 | Barrow vs Leyton Orient | 2.66 | 3.06 | 2.66 |
| 17:00 | 3087 | Peterhead vs Elgin City | 1.78 | 3.68 | 3.78 |
| 17:00 | 3291 | Sheffield Wed vs Wycombe | 1.64 | 3.70 | 5.00 |
| 17:00 | 3312 | Peterborough vs Port Vale | 1.91 | 3.45 | 3.75 |
| 17:00 | 3461 | Sutton United vs Salford City | 2.34 | 3.25 | 2.90 |
| 17:00 | 3524 | Shrewsbury vs Burton | 1.98 | 3.35 | 3.60 |
| 17:00 | 3824 | FK Radnicki Beograd vs FK Trajal | 2.39 | 2.89 | 2.99 |
| 17:00 | 4054 | Doncaster vs Crawley Town | 2.13 | 3.35 | 3.20 |
| 17:00 | 4072 | Grimsby vs Swindon Town | 2.23 | 3.30 | 3.05 |
| 17:00 | 4322 | Morecambe vs Cambridge Utd | 2.91 | 3.21 | 2.36 |
| 17:00 | 4857 | Bristol Rovers vs Accrington | 2.70 | 3.40 | 2.41 |
| 17:00 | 4903 | FK Loznica vs FC Rad | 2.41 | 2.76 | 3.11 |
| 17:00 | 5230 | Barnsley vs Charlton | 2.30 | 3.20 | 3.00 |
| 17:00 | 5598 | FC Chiasso vs Basel II | 1.76 | 3.94 | 3.59 |
| 17:00 | 5989 | Buckie Thistle FC vs Linfield Belfast | 5.12 | 4.14 | 1.51 |
| 17:15 | 2730 | Mirandes vs Zaragoza | 2.85 | 3.10 | 2.46 |
| 18:00 | 1955 | Longford Town vs Treaty United | 1.72 | 3.63 | 4.12 |
| 18:00 | 4525 | Finn Harps vs Bohemians FC | 3.44 | 3.34 | 1.96 |
| 19:00 | 1044 | Metalac vs FK Zlatibor | 1.43 | 4.20 | 7.00 |
| 19:00 | 3726 | Slovenia vs Norway | 3.84 | 3.43 | 1.93 |
| 19:00 | 4919 | Ivory Coast vs Togo | 1.80 | 3.42 | 4.69 |
| 19:00 | 5136 | Northern Ireland vs Kosovo | 2.22 | 3.23 | 3.23 |
| 19:30 | 4793 | Malaga vs Villarreal B | 2.20 | 3.20 | 3.20 |
| 19:30 | 5240 | Ponferradina vs Tenerife | 2.75 | 3.10 | 2.55 |
| 21:45 | 1470 | Czech Republic vs Portugal | 4.34 | 3.58 | 1.79 |
| 21:45 | 2315 | Serbia vs Sweden | 1.89 | 3.48 | 3.93 |
| 21:45 | 3067 | Spain vs Switzerland | 1.48 | 4.14 | 6.46 |
| 21:45 | 3877 | Israel vs Albania | 2.33 | 3.22 | 3.02 |
| 21:45 | 4639 | Scotland vs Ireland | 2.06 | 3.17 | 3.73 |
| 21:45 | 5310 | Cyprus vs Greece | 5.68 | 3.65 | 1.61 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumamosi Septemba 24, 2022
Nipashe

UKURASA 30



## Rashford, Dalot kupewa mikataba mipya




Bondia, Twaha Kiduku (kushoto) akiwa na mpinzani wake kutoka Misri, Abdo Khaled wakishikilia mkanda wa UBO ambao wanauwania katika pambano la kimataifa litakalofanyika leo kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona, Mtwara. **PICHA: SAADA AKIDA**

# Nabi awaandalia 'suprise' Al Hilal FC

●●●Lengo ni kuhakikisha Yanga inamaliza kazi nyumbani, Simba hawapoi...

**Na Saada Akida, MTWARA**

WAKATI ikijiandaa kuwakabili Ruvu Shooting, Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, amesema kikosi chake kina kibarua kigumu katika mechi yake ya raundi ya kwanza ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal kutoka Sudan itakayochezwa Oktoba 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Nabi, raia wa Tunisia alisema wachezaji wake wanatakiwa kuongeza juhudi kuelekea mechi hiyo na anahitaji kuona kila mcheza ameimarika zaidi ili wafikie malengo.

Nabi alisema, Yanga inatakiwa kupambana kwa nguvu zote kwa sababu katika mechi hiyo wanakutana na wachezaji na kocha ambaye ana uzoefu wa mashindano hayo yanayoandaliwa kila mwaka na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

"Ninajua wazi hatua inayofuata tutakuwa na kibarua kigumu, tunatakiwa kujipanga kwa ajili ya kwenda kushindana, nimepanga kukisuka kikosi imara ambacho kutakuwa tofauti na kile kimezoeleka katika michezo ya hivi karibuni.

Kocha huyo alisema anatarajia 'kufumua' kikosi chake na kusuka kikosi kazi kipya ambacho anaamini kitasaidia kuwavusha katika hatua inayofuata ya mashindano hayo ya kimataifa na vilevile kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Ninaufahamu ubora wa Al Hilal, nimeshaanza kufanyia kazi mambo ya kiufundi kwa ajili ya kufanikisha tunapata matokeo bora, nitahakikisha kikosi kitakachocheza na Al Hilal kitakuwa tofauti kabisa na kile kilichocheza mechi ya awali dhidi ya Zalan FC," alisema Nabi.

Aliongeza naye, ameshawafanyia upelelezi Al Hilal kupitia mechi zake mbili zilizopita dhidi ya St.George na kuona ubora wa wapinzani hao ambao umepelekea yeye kubadilisha mfumo na kwa kuanza na kupangua kikosi.

"Hatua inayofuata itakuwa ngumu kwa sababu tutakutana na watu bora kama sisi, najua tutakachofanya, tutaingia na mfumo tofauti kabisa, kuanzia nidhamu yetu na upangaji wa kikosi," alisema Nabi.

Aliongeza mechi haitakuwa rahisi kwa sababu pande zote mbili zimesajili wachezaji wazuri na zinahitaji kusonga mbele.

"Mechi hii tutaingia tofauti na tulivyocheza hivi karibuni, kila mchezaji atafanya majukumu yake kulingana na program ya mazoezi, kikubwa kuendelea kuwasisitiza washambuliaji kuwa makini wanapokuwa katika eneo la mpinzani ili kutafuta ushindi hasa katika mechi yetu ya nyumbani," Nabi alisema.

Aliongeza maandalizi yao yanayoendelea yanautizama pia mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ruvu Shooting utakaopigwa Oktoba 3, mwaka huu.

INAENDELEA UK. 31

## Stars majaribuni, U-23 yabanwa

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), kinatarajia kuwakabili Uganda (Uganda Cranes), katika mechi ya kirafiki ya kimataifa itakayochezwa leo ugenini nchini Libya.

Kaimu Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Honour Janza, aliliambia gazeti hili wachezaji wake wako tayari kwa mchezo huo ambao anaamini utawasaidia kuwajenga nyota wake wapya ambao wanahitaji kupata uzoefu.

Janza alisema anaamini atapata matokeo mazuri katika mechi hiyo na vile vile itakuwa kipimo sahihi kwake kuendelea kuwafahamu nyota wake lakini pia akijipanga kuimarisha pale atakapoona kuna mapungufu.

"Nina furaha tumepata nafasi nyingine ya kukutana na Uganda, ninaamini wachezaji wangu wataonyesha mchezo mzuri, si kwa sababu walitufunga katika mechi zilizopita, lakini watataka kurekebisha pale walipokosea, utakuwa mchezo mzuri kwetu sote," Janza alisema.

Aliongeza anatarajia kutumia mechi hiyo kwa ajili ya maandalizi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika.

"Kama nilivyosema Machi (mwakani), tutakuwa na mechi za kusaka tiketi ya kushiriki fainali za AFCON, hii ni sehemu nzuri ya kujiimarisha kuelekea mashindano hayo makubwa yaliyoko mbele yetu, najua haitakuwa mechi nyepesi, lakini ninawaamini wachezaji wangu wataongeza umakini," aliongeza kocha huyo aliyechukua mikoba wa Kim Poulsen.

Stars itashuka tena dimbani Jumanne kuwakabili wenyeji Libya katika mchezo mwingine wa kirafiki wa kimataifa ulioko kwenye kalenda ya FIFA.

Wakati huo huo, Timu ya Soka ya Taifa ya umri chini ya miaka 23 imetoka sare ya bila kufungana na Sudan Kusini katika mechi ya kwanza ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON U-23) iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana.

Hadi mapumziko timu hizo zilikuwa hazijafungana katika mchezo

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002